Jumanne Januari 14, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581921
www.ippmedia.com 0677 020 710 MWANGA WA JAMII
Nipashe digital
LIKE & FOLLOW US
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ
epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com



UKURASA 22
**AC MILAN YAONGOZA KUMTWAA WALKER**

UKURASA 8
**Tanzania** kutumia Mkutano wa Nishati kumaliza kilio cha umeme kufikia 2030

UKURASA 18
**TLS** yataja dawa kufuta matukio ya utekaji watu

UKURASA 19
**Mtanzania** aliyetekwa nyara Kenya aachiliwa

# Mbowe: Kuangamiza CHADEMA ni uhaini

• **Aja** na hoja kukosoa viherehere, shetani anayewaandama; Lissu naye afunguka... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Baraza la Vijana wa chama hicho (BAVICHA), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mawakili wa Serikali: Hatujui aliko Dk. Slaa

UKURASA 3



## CCT yakosoa utitiri vibali kwa wafanyabiashara

UKURASA 18

**MICHEZO** FADLU SASA ATAKA UKINARA WA KUNDI UK.24 **MAONI,** UK.6

# Mbowe: Kuangamiza CHADEMA ni uhaini

**Na Elizabeth Zaya**

HUKU kukiwa na kauli tofauti juu ya hatima ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) dhidi ya mchakato unaoendelea wa uchaguzi wa viongozi wakuu, Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Freeman Mbowe amesema kuangamiza chama hicho hakuna tofauti na uhaini kwa kuwa kimebeba maono ya watanzania wengi.

Amesema kuwa kila mwanachama wa chama hicho anapaswa kumkataa shetani anayetaka kukifarakanisha chama hicho.

Mbowe alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Baraza la Wazee wa Chama hicho (BAZECHA) ambao ulitumika kuchagua viongozi wapya wa baraza hilo.

Mbowe alisema chama hicho ni bora na kikubwa kuliko mtu yeyote, awe kiongozi wa kitaifa, kwenye mabaraza yake au mwanachama.

Alisema yapo mambo mengi ambayo wamejifunza katika kipindi chote cha mchakato wa uchaguzi huo, akiweka wazi kuwa tabia iliyojionyesha katika uchaguzi wa awamu hii si tabia za wana-CHADEMA waliojenga chama hicho kwa jasho na damu kwa zaidi ya miaka 30.

"Yako mengi ya kujifunza, tumeona minyukano ikitokea kwenye mitandao, miongoni mwa wanachana na viongozi, lakini ninachotaka kuwahusia wanachama wetu ni kwamba chama hiki ni bora na ni kikubwa kuliko yeyote miongoni mwetu. Kwa hiyo kila kiongozi bila kujali nafasi yake ndani ya chama au ndani ya mabaraza ana wajibu wa kukilinda," alisema.

Mbowe alisema anaamini chama hicho kitakuwa bora na kuimarika zaidi kama kitalindwa kwa umoja wao.

Alisema kuna baadhi ya watu ambao siyo wanachama wa chama hicho ambao wanashabikia kile kinachoendelea ndani na kuwataka wanachama wa chama hicho kukataa kuingia katika mtego wao.

"Tumkatae shetani na mbinu zake zote, wako wengine ambao siyo wana-CHADEMA, wana kiherehere na mambo ya CHADEMA, kuliko tulivyo wanachama, tukatae tuseme umoja wetu ni wa muhimu kuliko sifa ya mtu yeyote miongoni mwetu mmoja mmoja," alisisitiza Mbowe.

**ALIVYOKABIDHIWA CHAMA**

Mbowe alitumia jukwaa hilo kuwasimulia wajumbe hao namna alivyokabidhiwa chama hicho kukiongoza kwa mara ya kwanza mwaka 2004 katika nafasi anayoishikilia hadi sasa, huku akigusia alivyofanya mabadiliko.

"Nilipokabidhiwa chama hiki mwaka 2004, kilikuwa hakina mabaraza, kulikuwa kuna kamati ya taifa ya vijana na kamati ya taifa ya kinamama. Wakati wazee wananikabidhi, niliwaambia kwamba kama mnataka niwe kiongozi wa chama hiki, nitafanya mabadiliko makubwa ya Katiba ya chama, tuingize mawazo, mikakati ya kukipanua chama hiki.

"Wakati ninakabidhiwa hata bendera yetu ilikuwa ya rangi moja, kwa hiyo tukakubaliana kwamba tunabadilisha Katiba, tukaanzisha mabaraza ya chama, kulikuwa hakuna kanuni ya uendeshaji, hakukuwa na itifaki lakini haya yote tuliyapata si kwa ajili ya Mbowe, ni kwa sababu tulifanya kazi katika umoja wetu, tukiweka mawazo yetu pamoja," alisema.

Mbowe alisema hata sasa bado ipo nafasi ya kila mwanachama wa chama hicho kutoa mawazo yake ya namna anavyoona chama hicho kinaweza kufanyiwa maboresho kulingana na Katiba inayokiongoza.

"Hata leo tuna wajibu wa kuweka mawazo yetu pamoja, yeyote miongoni mwetu anayefikiria kuna mambo yakifanyika, yatakifanya chama hiki kiwe bora zaidi, milango iko wazi, hatuna sababu ya kulumbana. Kama kuna mambo ya kurekebisha tufanye kwa namna ambavyo Katiba yetu imeruhusu kwa umoja, upendo, kwa kushirikishana.

"Haya yote yanawezekana kwa sababu chama cha siasa, Katiba, kanuni, maadili na miongozo yake ni nyaraka zinazoishi wala si kama vitabu vitukufu vya Mungu ambavyo vikiandikwa haviwezi kubadilishwa kila siku," alisema Mbowe.

Alisema kama dunia inaishi na mabadiliko, hata chama kinaweza kufanya maboresho, hivyo CHADEMA nacho kinaweza kufanya hivyo.

"Dunia inaishi, yanatokea mabadiliko ya kiteknolojia, ya kijamii na kiuchumi ambayo yanapelekea ulazima wa kufanya rejea na kurekebisha mambo kadri muda unavyokwenda na mahitaji ya wakati.

"Kwa hiyo tusitafute sababu yoyote ya kuleta ugomvi miongoni mwetu, kila mmoja ailinde taasisi hii, tunapoona kuna cha kurekebisha, tushauriane, turekebishane kujenga umoja na mshikamano wetu," alisema Mbowe.

Mwenyekiti huyo pia alionya tabia ya vijana wa chama hicho kuwabeza wazee waliotumikia chama hicho.

"Juzi nilikuwa ninaongea na vyombo vya habari, nikakemea tabia moja ambayo inaanza kujengwa na vijana kufikiri uzee ni laana na kutokuuona kama busara, kutokuuona kama uzoefu na kutokuona uzee kama maktaba ya chama, kwamba tunaweza kuwa na ujasiri wa kuwahukumu viongozi ambao wana umri mkubwa katika chama chetu.




Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Vijana wa chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"Kwamba tukishafikia umri wa kustaafu, ninyi wazee hamna thamani ndani ya chama hiki, haiwezekani! Ngoma ya watoto haikeshi, ninataka wakati wetu tuwatambue wazee," alisema Mbowe.

**NIDHAMU**

Mbowe pia alisema chama hicho hakiwezi kujengwa kuwa imara kwa matusi na kukashifiana bali kitafanikiwa endapo kutakuwa na nidhamu.

"Hatuwezi kujenga chama cha ukombozi wa nchi kama kila mmoja hawezi kumwona mwenzake kama bega la kulilia katika mapambano, si kweli kwamba kutwezana, kutukanana, kukashifiana, kudhalilishana, kunaweza kuwa sehemu ya kukijenga chama imara. Leo nilikuwa namwuliza (Tundu) Lissu kwamba hawa vijana wa moto kwelikweli, hivi walizaliwa mwaka gani?

"Kwa waliokuwapo miaka 30 ya ujenzi wa chama walishirikiana, walijengana, lakini kwa tabia iliyooneshwa kwenye uchaguzi wa awamu hii, si utamaduni wa CHADEMA.

"Mtambue kwamba kila mmoja wenu anamwitaji mwingine, tunahitajiana wote kama familia ili kutimiza malengo yetu, pepo lolote lenye dhana ya kutuntenganisha hatupaswi kulilea, lishindwe kwa nguvu zote," alisema Mbowe.

Mwenyekiti huyo alisema ni sahihi kutofautiana pindi uchaguzi unapokaribia, lakini ni vyema pia watu wakaimarisha umoja wao.

Mbowe alisema: "Ni kweli tutanyukana, tukaonana kwenye boksi lakini tukimaliza lazima tushikane mikono kutafuta fomula kwamba tunahitajiana, tunataka chama hiki watoto wa watoto wenu wakakikute kikiwa imara kuliko jana na si kwa kutukanana.

"Tuinue taasisi hii ambayo iliundwa kwa jasho, damu na machozi ya watu. Hatupaswi kuendekeza hili, hivi vyeo vinapita, malengo yetu ni ya msingi kuliko nafasi ya kila mmoja wetu, tunawahitaji wazee, tunawahitaji vijana jeuri, tunawahitaji wazee imara, tunahitaji kinamama, tunahitajiana, tupendane tuvumiliane, tuijenge familia ya CHADEMA."

**TUNDU LISSU**

Naye Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Lissu, alisema vijana ndiyo nguvu ya mabadiliko na kuwataka wachague viongozi ambao watakuwa jasiri watakaoongoza mapambano pasipo kukimbia pindi mambo yanapokuwa magumu.

Akizungumza katika mkutano wa BAZECHA, Lissu aliwataka wajumbe hao kuwachagua viongozi ambao watawaongoza vyema na kwa haki katika miaka mitano ijayo.

"Niwatakie kila la heri katika uchaguzi huu, tuchague viongozi watakaotuongoza vyema katika miaka mitano inayokuja, tuchague viongozi kwa uchaguzi ulio huru, wa haki na wa wazi kama yanavyosema maneno ya Katiba yetu," alisema Lissu.

Mwanazuoni Dk. Azaveli Rwaitama aliwaonya wapambe wanaoshabikia wagombea katika uchaguzi huo, akisema watu hao ni hatari kuliko wagombea wenyewe.

Pia alitoa hadhari kwa atakayechaguliwa kuwa mwenyekiti wa chama hicho kuepuka kiburi.

Uchaguzi wa viongozi wa ngazi za juu wa chama hicho unatarajiwa kufanyika Januari 21 mwaka huu, huku macho na masikio ya wengi yakielekezwa kwa atakayeshinda nafasi ya uenyekiti, Mbowe na Lissu wakiwa miongoni mwa wanaoiwania.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Mawakili wa Serikali: Hatujui aliko Dk. Slaa

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kusambaza taarifa za uongo kupitia mtandao wa X inayomkabili mwanasiasa mkongwe, Dk. Wilbroad Slaa umedai haujui aliko mshtakiwa huyo na pia haujui sababu za kutokupelekwa mahakamani.

Jopo la mawakili watano wanaomtetea Dk. Slaa, akiwamo Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Boniface Mwambukusi, limedai kushangazwa na Jamhuri kutokujua aliko mshtakiwa wakati wao walizuia dhamana yake kwa madai ya kulinda usalama wake.

Kesi hiyo iliendelea kwa mabishano mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Beda Nyaki wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuanzia saa 5:12 asubuhi hadi saa 6:22 mchana bila mshtakiwa kuwapo, hoja mbalimbali ziliibuliwa ikiwamo uhalali wa mashtaka.

Kutokana na mabishano hayo makali ambayo yalikuwa hayana mwafaka kwa pande zote mbili, Hakimu Nyaki alifikia uamuzi wa kuwaita mbele mawakili wote 11 ili wazungumze kwa utaratibu wa kuelewana kwa pande zote.

Hata hivyo, mawakili hao waliporudi kwenye viti vyao, minong'ono ya chini ikiendelea na walipopewa nafasi ya kuzungumza mabishano yaliendelea ya kusikilizwa kwa kesi hiyo bila mshtakiwa kuwapo, utetezi wakitaka iendelee ilhali Jamhuri wakipinga hilo.

Mbali na Mwambukusi, mawakili wengine ni Peter Madeleka, Hekima Mwasipu, Sanga Melikiole na Sisty Aloyce ambao wote wanamwakilisha Dk. Slaa huku wakidai afya yake si nzuri kukaa mahabusu, anatakiwa awe chini ya uangalizi wa familia yake.

Jopo la Mawakili wa Serikali linaongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Tawabu Issa, Clemence Kato, Michael Ngoboko, Nura Manja, wakisaidiana na Mawakili wa Serikali Abdon Bundala na John Mwakifuna, walipinga kesi kuendelea kusikilizwa kutokana na maombi yalikuwa mahakamani.

Baada ya utambulisho wa mawakili wa pande zote, Hakimu Nyaki aliuliza alikokuwa mshtakiwa. Wakili Issa alidai kwamba wao kesi ilipoitwa walijua yupo na hawakupata sababu za kutofikishwa mahakamani.

"Ninyi ndio mmemleta mahakamani, ndio mmezuia dhamana yake kwa sababu ya usalama wake na amri ya mahakama leo alitakiwa awapo mahakamani, lakini cha kushangaza na wao wanashangaa kutokuwapo kwake, huo usalama wanaosema uko sehemu gani?

"Wenye wajibu wa kumleta ni wao, hatujaja hapa kuleta utani, tunaomba wawajibike kwa hili," alidai Wakili Madeleka.

Hakimu Nyaki akahoji 'hatuwezi kuendelea bila yeye kuwapo (Dk. Slaa)?. Wakili Mwabukusi akadai "tunaomba tuendelee bila yeye kuwapo. Mahakama iweze kutoa uamuzi kwa sababu ina uwezo wa kusikiliza jambo hili bila kuwapo mtuhumiwa."

Akijibu hoja hiyo, Wakili Issa alidai wamesikia mawasilisho ya kuendelea na kesi hiyo bila mshtakiwa kuwapo, lakini kumbukumbu za mahakama zinaonesha kuna pingamizi la dhamana.

"Yaliyowasilishwa ni mambo kwa kuwa tuliyawasilisha kwa hati ya faragha na kiapo tulitegemea kupata kiapo kinzani kutoka kwa mjibu maombi Dk. Slaa kisha tupangiwe tarehe nyingine ya kusikilizwa," alidai Wakili Issa.

Akijibu hoja hiyo, Wakili Madeleka alidai hoja ya kuendelea au la tayari Mwambukusi ameomba kuendelea bila Dk. Slaa kuwapo kwa sababu hakuna sheria inayokataza hilo.

"Tupo tayari kusikiliza maombi ya dhamana na pia tupo tayari kusikiliza maombi madogo yaliyofunguliwa," alidai.

Baada ya Hakimu Nyaki kusema kwamba kesi itasikilizwa kwa siku tatu mfululizo, Wakili Mwambukusi alidai Dk. Slaa amekamatwa na kushtakiwa kinyume cha sheria, anaomba isikilizwe hata usiku kutokana na afya yake kwa sababu hajapatikana na hatia.

"Mheshimiwa, kesi hii tunayozungumzia mshtakiwa yupo mahabusu, si uraiani, tunaomba tusikilizwe kwa njia ya mdomo na si kwa maandishi kwa sababu ya muda," alidai.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri ulidai kuwa hauwezi kuendelea na usikilizwaji huo wa maombi ya dhamana, ambapo Wakili Madeleka akidai wanaweza kuendelea. Wanaomba isikilizwe Jumatano ya wiki hii.

"Hatuna shida ya juu ya usikilizwaji lakini na sisi tuna mapendekezo yetu ni tarehe ya usikilizwaji angalau iwe Ijumaa kwa sababu mawakili wengi hapa watakuwa kwenye kesi zingine za uhujumu uchumi," alidai Issa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Januari 17, 2025 saa tatu asubuhi kwa ajili ya kusikilizwa.

Hata hivyo, Wakili Madeleka aliwasilisha pingamizi la kutokuwa na uhalali wa hati ya mashtaka kwa sababu sheria inaeleza kwamba upelelezi ukikamilika ndipo mshtakiwa apelekwe mahakamani, lakini Dk. Slaa alifikishwa mahakamani bila upelelezi kukamilika.

Ilidaiwa kuwa Dk. Slaa alitenda kosa hilo Januari 9, mwaka huu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mtandao huo wa kijamii, akitumia jukwaa lililosajiliwa kwa jina la Maria Salungi Tsehai @ MariaSTsehai kwa lengo la kupotosha umma.

Ilidaiwa kuwa kupitia jukwaa hilo, Dk. Slaa alichapisha ujumbe uliosomeka "wakubwa wametafutana, nikisema wakubwa ninamaanisha Mwamba na Samia, na wala hatuna maneno ya kumung'unya... na kimsingi wamekubaliana, Suluhu Samia amekubali atatoa pesa, Suluhu Samia amekubali ataongeza nguvu ya pesa, ni dhahiri atatoa pesa... hizo ni hela za watanzania wanazichezea Samia na watu wake.

"Samia toka muda mrefu haangaikii tena maendeleo ya nchi, anahangaikia namna ya kurudi Ikulu, na namna yake ya kurudi Ikulu ni kwa njia hizo kama kumsaidia mtu kama Mbowe."

Upande wa Jamhuri ulipinga ombi hilo la upande wa utetezi ukidai umewasilisha kiapo kupitia mfumo wa mahakama kupinga dhamana ya mshtakiwa huyo kilichoapwa na SSP George Bagyemu.

# Kesi ya mauaji ya mtoto kutajwa Januari 27

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

KESI ya mauaji ya kukusudia ya mtoto Greyson Kanyenye (6), aliyekuwa akiishi Ilazo, jijini Dodoma, inayowakabili washtakiwa Kelvin Joshua (27) ambaye ni dereva bodaboda na Tumaini Msangi (28), bondia, imeahirishwa hadi Januari 27, mwaka huu itakapotajwa tena.

Washtakiwa hao wawili walifikishwa kwa mara ya kwanza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma Desemba 30, 2024 kwa kosa la kuua kwa kukusudia tukio lililotokea mtaa wa Ilazo jijini Dodoma, Kata ya Ipagala Desemba 25, mwaka jana.

Hakimu Mkazi Daraja la kwanza, Charles Eligy, aliahilisha kesi hiyo jana hadi Januari 27, mwaka huu itakapotajwa tena huku washtakiwa wote wawili wakiendelea kusota mahabusu kutokana na kosa lao kukosa dhamana.

"Shauri hili linaahirishwa hadi Januari 27, mwaka huu litakapotajwa tena na washtakiwa wote wawili mtaendelea kubaki mahabusu kutokana na kosa lenu halina dhamana," alisisitiza Hakimu Eligy.

> **"Shauri hili linaahirishwa hadi Januari 27, mwaka huu litakapotajwa tena na washtakiwa wote wawili mtaendelea kubaki mahabusu kutokana na kosa lenu halina dhamana," alisisitiza Hakimu Eligy.**

Awali, Wakili Mwandamizi wa Serikali, Patricia Mkina, aliiambia mahakama hiyo kuwa kesi hiyo ilikuja jana kwa ajili ya kutajwa na upelelezi bado unaendelea.

"Mheshimiwa hakimu shauri hili lilikuja leo mbele yako kwa ajili ya kutajwa na upelelezi bado unaendelea hivyo kwa ridhaa yako tunaomba utupangie siku nyingine kwa ajili ya kutajwa tena," alisema Mkina.

Desemba 30, mwaka jana, Wakili Mkina akisoma hati ya mashtaka, alisema washtakiwa wote wawili walifanya kosa la mauaji ya Greyson Desemba 25, 2024.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo Hakimu Mkazi Denis Mpelembwa, alisema mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza mashauri ya mauaji.

"Kosa la mauaji halina dhamana hivyo mtarudi mahabusu hadi kesi yenu itakapotajwa tena Januari 13, 2025," alisema Hakimu Mpelembwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, akizungumzia tukio hilo Desemba 25, 2024, alisema mwili wa mtoto huyo ulikutwa ndani ya nyumba ukiwa na majeraha shingoni.

Katabazi, alisema tukio hilo lilitokea majira ya saa 1:00 asubuhi katika mtaa wa Bwawani, Ilazo Extension jijini Dodoma, nyumbani kwa Ofisa Uvuvi wa Mtera, Hamis Mohamed.

Alisema, Hamis na mama wa mtoto huyo walitoka kwenda matembezini na kumwacha chini ya usimamizi wa dereva bodaboda maeneo ya Ilazo, Kelvin Joshua.

Alisema, inadaiwa kuwa bodaboda huyo walimfahamu kupitia huduma ya usafiri anayoitoa kwa familia hiyo.

"Bodaboda huyu aliachiwa mtoto ili amwangalie kipindi ambacho watakuwa kwenye matembezi wawili hao wakati wa usiku, lakini waliporudi mtoto hawakumwona hadi asubuhi majira ya saa 1:00 walipomkuta mtoto kwenye chumba akiwa ameuawa akiwa na alama za kupigwa na kitu kizito shingoni," alisema.

Kadhalika, Kamanda Katabazi alisema Jeshi la Polisi mkoani hapa linamshikilia bodaboda huyo kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa tukio hilo.

"Tumemkamata bodaboda huyo kwa ajili ya uchunguzi wa tukio hili ambapo yeye amekanusha kuhusika na jambo hili, lakini tunaendelea na uchunguzi ili kubaini nini hasa kilitokea kwa mtoto huyu na kupelekea kifo chake," alisema Katabazi.

Aidha, kamanda huyo alitoa wito kwa wazazi kuacha tabia ya kukabidhi watoto wao kwa watu ambao hawawajui vizuri ili kuepusha matukio kama hayo.


**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**HARID KASSIMU MAYUHANA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI MC 743 CAD. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **PHQ/MBE/MBE/1624/2025.**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**IRENE JULIUS MTEI** anatangaza kupotea kwa vyeti BACHELOR OF SCIENCE IN DIALYSIS TECHNOLOGY DEGREE pamoja na TRANSCRIPT vyenye Namba: 126232, vilivyotolewa Chuo cha SHARDA UNIVERSITY INDIA mwaka 2023 . Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No:9910843723102

**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**MWASITI MUSTAPHA SALIMU** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria yenye namba TAE283639 iliyotolewa Uhamiaji Makao Makuu mnamo tarehe 17/01/2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/7263/2025.**

**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**MATHIAS MASELE KAJI** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba TAE 626805 iliyotolewa uhamiaji makao makuu Idara ya Uhamiaji tarehe 22 August, 2023. Yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: PHQ/SHI/SHI/328/2025**

## Kesi jengo lililoporomoka Kariakoo yapigwa kalenda

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa mashtaka katika kesi ya kuua bila kukusudia inayowakabili wanaodaiwa kuwa ni wamiliki wa jengo la ghorofa Kariakoo liliporomoka na kusababisha vifo vya watu 31, umedai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

Washtakiwa hao ni Leon Leondela Mdete (49), mkazi wa Mbezi Beach; Zenabu Islam (61), mkazi wa Kariakoo; na Ashour Awadh Ashour (38), mkazi wa Ilala. Washtakiwa wote ni wafanyabiashara.

Taarifa hiyo ya hatua ya upelelezi ilitolewa jana na Wakili wa Serikali Roida Mwakamele mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Gwantwa Mwankuga hiyo wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

"Kesi ilikuja kwa ajili ya kutajwa na upande wa mashtaka bado unaendelea na upelelezi, hivyo tunaomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia," alidai Mwakamele.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Februari 10, 2025 kwa kutajwa.

Inadaiwa washtakiwa hao Novemba 16, 2024 katika Mtaa wa Mchikichi na Congo, Kariakoo jijini Dar es Salaam, isivyo halali, kwa pamoja walishindwa kutimiza majukumu na kusabashisha vifo vya watu 31.

Waliofariki dunia ni pamoja na Said Juma, Hussein Njou, Prosper Mwasanjobe, Shadrack Mshingo, Godfrey Sanga, Neema Sanga, Elizabeth Mbaruku, Hilary Minja, Abdul Sululu na Chatherine Mbilinyi.

Wengine ni Elton Ndyamkama, Mariam Kapekekepe, Elizabeth Kapekele, Hadija Simba, Frank Maziku, Rashid Yusuf, Ally Omary, Ajuae Iyambilo, Mary Lema, Khatolo Juma, Sabas Swai, Pascal Ndungulu, Brighette Mbembele, Ashery Sanga, Venance Aman, Linus Hasara, Issa Bakari, Lulu Sanga, Happnees Malya na Brown Kabovera.

Baada ya washtakiwa kusomewa mashtaka hayo, hakimu aliwaeleza washtakiwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi yao, hivyo hawatakiwi kujibu lolote.

Washtakiwa wako nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya dhamana ambayo ni kuwa na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho, kitambulisho cha taifa na kutia saini bondi ya Sh. milioni tano kwa kila mmoja.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (wa pili kulia), akipokea sehemu ya msaada wa vifaa vya afya kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Juma Kimori (wa tatu kushoto), wakati wa hafla ya uzinduzi wa Tawi la NMB Wete lililoko Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kulia ni Naibu Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hamad Hassan Chande, kushoto ni Meneja wa NMB Kanda ya Zanzibar, Naima Said Shaame na wa pili kushoto ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Milioni 100/- zasaidia elimu, afya Wete

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amezindua Tawi la NMB Wete katika Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, huku akiahidi kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) itaendeleza ushirikiano wake na NMB, benki aliyoitaja kama kinara wa kuunga mkono jitihada za utekelezaji miradi mikubwa na ya kimkakati.

Uzinduzi wa NMB Tawi la Wete umefanyika Januari 10 na kuhudhuriwa na viongozi wa Serikali, akiwamo Mkurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) - Kanda ya Zanzibar, Ibrahim Malogoi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango wa Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum na Ofisa Mkuu wa Fedha NMB, Juma Kimori.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Makamu wa Rais alisema tawi hilo ni muhimu kwa ustawi na maslahi mapana ya wananchi wa Kaskazini Pemba na Zanzibar kwa ujumla na kwamba mwitikio wa haraka wa wateja 1,800 waliofungua akaunti zao baada ya kufunguliwa unaakisi kiu ya maendeleo ya wakazi wa eneo hilo.

"Uzinduzi huu wa NMB Wete, ni jambo muhimu kwa maisha maslahi ya wananchi wa Kaskazini Pemba na Wazanzibar, takwimu zimetolewa hapa kuwa siku chache kabla uzinduzi huu wateja 1,800 wamefungua akaunti, hii ni kuthibitisha kiu yao ya huduma zenu, ndio maana ninasisitiza wananchi wachangamkie fursa.

"Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB ameeleza fursa nyingi na huduma nyingi watakazotoa hapa, nami nieleze kuwa wananchi karibieni tawini mjue huduma na fursa hizo na mzitumie.

"Ninasisitiza hilo huku nikiwaomba NMB waendelee kusambaza na kuboresha huduma zao kwa wananchi, hasa suala zima la huduma za kidijitali," alisema Makamu wa Rais.

Aliongeza kuwa SMZ inaahidi ushirikiano mkubwa na NMB katika kufanikisha ustawi na maisha bora kwa Wazanzibar, akibainisha kuwa ubora wa huduma unaooneshwa na benki hiyo unatokana pia na mazingira mazuri na uwekezaji mzuri wa teknolojia uliofanywa.

"Ujio wa NMB Wete utaleta na kuchachua ushindani wa taasisi za fedha Kaskazini Pemba katika huduma, ambazo hazihitaji ushawishi wa maneno, bali huduma zenyewe ndio mshawishi mkuu," alisisitiza Abdullah huku akituma salamu za pongezi kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Ruth Zaipuna kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya.

"Kwa dhati kabisa shukrani zetu zimfikie CEO wa NMB, na salam zimfikie, tunamshukuru kwa ushirikiano wake na sapoti zake kwa SMZ na hata Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hakika amekuwa mfano wa kuigwa, kazi kubwa anaifanya na tunampongeza kwa juhudi zake, utumishi na ushirikiano wake.

"Mambo mbalimbali yamesemwa jinsi waliyosaidia hapa Pemba, leo tunapokea msaada mwingine wa vitanda kwa hospitali ya Mzambarauni lakini kwa hospitali ya Kendwa tayari vimeshafika na kwa kweli vinafanya kazi na kutusaidia sana," alihitimisha.

Awali Mkuu wa Fedha wa NMB, Juma Kimori kwa niaba ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna, alishukuru SMZ na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano bora inaoonesha kwa NMB na mazingira wezeshi inayoyaimarisha kila uchao katika kuwezesha taasisi za fedha kuhudumia wananchi kwa ufanisi.

"Tuko hapa kuthibitisha kwa vitendo kaulimbiu yetu ya 'Karibu Yako', NMB Wete inakwenda kumaliza adha ya wakazi wa hapa kusafiri umbali wa kilomita zaidi ya 30 kwenda Chakechake kufuata huduma za kibenki na sasa watapata huduma zote hapa tawini ikiwamo mikopo, kuweka na kutoa pesa, bima na kubadilisha fedha.

"NMB Wete ni miongoni mwa matawi 241 kote nchini na tisa kwa visiwani Zanzibar. Hii maana yake ni kwamba mtandao wetu wa huduma unaojumuisha ATM 720, kati ya hizo, 22 zikiwa hapa Zanzibar, unaendelea kukua kwa kasi na ahadi yetu ni kuzidi kusogeza huduma kwa Watanzania wote, kote nchini.

"Tunaahidi kuendelea kusafiri pamoja na serikali zote, hasa SMZ katika meli yake ya uchumi wa buluu, sera ambayo ni muhimu mno kwa ustawi wa Wazanzibari.

"Sambamba na uzinduzi huu, tunakabidhi vitanda 10 vya kulaza wagonjwa, vitano vya kujifungulia na mashuka 80 kwa Hospitali ya Mzambarauni, vifaa tiba mbalimbali kwa hospitali ya Kendwa, vifaa vya uezekaji skuli za Tasini na Mwambe vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 110. Mkurugenzi wa BoT – Kanda ya Zanzibar, Ibrahim Joseph Malogoi, alipongeza NMB kwa jitihada kubwa inazofanya katika kusambaza huduma za kibenki kwa jamii, akiitaja ni miongoni mwa benki 14 zilizopo Zanzibar na nne zilizofikisha huduma kwa wananchi wa Pemba.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alipongeza NMB kwa kuzindua tawi jipya Wete, akisema ni mwendelezo wa taasisi hiyo kuunga mkono Sera ya Ujumuishwaji Wananchi katika masuala ya fedha. Kiwango cha watanzania wanaotumia huduma hizo imeongezeka kwa kasi.

# Waziri aagiza shule kuunda kamati za ulinzi wa watoto

**Na Halima Ikunji,** TABORA

SERIKALI imeagiza shule nchini kuunda kamati za ulinzi wa watoto ili kukabiliana na ukatili wa kijinsia na mmomonyoko wa maadili.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Doroth Gwajima alitoa maelekezo hayo juzi wakati akizungumza na wakazi wa Jimbo la Ulyankulu, Mkoa wa Tabora.

Dk. Gwajima alisema kukosekana kwa kamati hizo shuleni ni chanzo cha mmomonyoko wa maadili miongoni mwa wanafunzi, kufanyiwa vitendo vya ukatili na kushindwa kutimiza ndoto zao kwa siku za baadaye.

Alisema serikali ilitoa mwongozo wa kuundwa kamati hizo, hivyo ni muhimu utekelezaji uanze shule zinapofunguliwa mwezi huu ili watoto wasome na kuhitimu masomo yao wakiwa na maadili mazuri.

Alisema kamati hizo zitasaidia kumlinda mtoto dhidi ya ukatili na kuwaepusha kujiingiza katika michezo michafu ya ulawiti, mapenzi ya jinsia moja na matendo mingineyo yasiyofaa.

Aliwataka wazazi, walezi na jamii kukaa na watoto wao kuwafundisha maadili mema na jinsi ya kuepuka ukatili wa kijinsia. "Anapofanyiwa ukatili mtoto pamoja na kupokea mafunzo yanayokiuka maadili, ataharibika mapema na hataweza kutimiza ndoto za maisha yake, Ninaomba sana tuzingatie hili kujenga jamii iliyo bora," alisema.

Pia alionya kuwa ujenzi wa miundombinu na maboresho ya mazingira ya watoto kujifunzia yanayoendelea kufanywa na serikali, hayatakuwa na maana kama watoto wasipolindwa na kuziishi ndoto zao na hatimaye kuzifikia.

Mbunge wa Ulyankulu, Rehema Migira alisema jimbo hilo limepokea zaidi ya Sh. milioni 361 kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya ya Msingi Langoni ili kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule mama ya Ibambo. Vilevile, alisema jimbo hilo limepokea Sh. milioni 136 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Mkindo ili kupunguza adha ya kutembea umbali mrefu kwa wanafunzi na kuingia majaribuni.

# MATANGAZO


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: HSE METHODS AUDITS COORDINATOR-TZ**

**Reports to:** HSE METHODS AND AUDIT LEAD

**Job Type:** Full Time

**Location:** Dar-es-Salaam (TZ)

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

**CAPEX Project:** The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a major regional infrastructure project (Capex: 4.1 G$, OPEX:>2.5G$ over 25 years) between Uganda and Tanzania coast, opening a new value corridor between the two countries. The role does not have a direct budget function.

**Corporate HSE Department:** The role will be based within the Corporate HSE Department and will provide functional support to the Methods and Audits team. The role interfaces with the Project teams to integrate the contractor plans into the Corporate systems and strategies.)

### ACTIVITIES

- HSE Management System: Develop and implement the key processes and working tools/documents required for an effective EACOP HSE Management system (HSE-MS).
- Coordinate the EACOP Corporate HSE Audit program.
- Coordinate and implement the EACOP HSE training requirements.
- Conduct Contractor evaluation and audit.

### CONTEXT AND ENVIRONMENT

- Behind the numerous technical, environmental, and social challenges faced by the project, objective is for EACOP to be developed in a fast-track mode with start-up anticipated 39 months after FID.
- With operations in two countries, two separate regulatory regimes will need to be addressed in the HSE-MS.
- Numerous stakeholders and heavy focus by NGOs create a complex context. Project will need to be developed in accordance with IFC standards and the Equator 4 Principles to secure the necessary financing.
- Several risks related to the location including malaria, limited infrastructure, significant transport & road risk, etc.
- Job Location: The position is based at Dar es Salaam Office (Tanzania) and with travel to Uganda offices and worksites.

### ACCOUNTABILITIES

- Prepare the required documentation as outlined in the HSE management system, in line with the EACOP Integrated Management System (EIMS).
- Support the HSE Methods & Audit Lead to establish the processes required for the implementation of the HSE procedures in the EACOP Organization.
- Coordinate the EACOP Corporate HSE Audit program.
- Lead Auditor for internal and 3rd party Contractor HSE Audits.
- Conduct the HSE evaluation of contractors and support Contract Owners to develop and implement effective contractor oversight.
- Support and coordinate HSE Training requirements and delivery model for the Corporate functions.
- Perform any other duties or tasks that may be required by the position.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- Bachelor's degree and/or equivalent formal qualification in a recognized HSE discipline (NEBOSH Certificate or higher qualification).
- National Occupational Safety and Health OSHA certified (NOSHC Module I & II).
- Lead Auditor with qualification recognized by a certification body (i.e., IRCA, CQI). Registered expert for conducting environmental audits, with National Environmental Management Council (NEMC) for Tanzania is an asset.
- Minimum 10 years of experience in Oil & Gas Industry or related experience in large scale projects & industrial operations.

**Technical competencies:**
HSE Management system development expertise. Subject Matter Expert for Occupational Health and Safety; Certified Lead Auditor; Risk Analysis, Contractor HSE Management.

**Behavioral competencies:** Ability to work in a multi-cultural business setting and excellent interpersonal and communication skills essential. Fluent in English: Speaking and Writing.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 13th Feb 2025.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**



halotel

## TAARIFA KWA UMMA

Viettel Tanzania PLC (Halotel) ni kampuni ya mawasiliano inayoendelea kuboresha huduma na kuvunja mipaka ya mawasiliano kwa wateja wetu kwa kutoa gharama nafuu kwenye SMS, Huduma za kupiga simu na Intaneti.

Tunapenda kuwatangazia wateja wetu na umma kwa ujumla juu ya gharama zetu za makato pindi mteja atakapokuwa hajajiunga kwenye kifurushi.

### GHARAMA ZA NDANI YA NCHI

| Kipengele | Gharama |
|---|---|
| Kupiga Halotel kwenda Halotel | 10 Tsh/Dk |
| Kupiga Halotel kwenda mitandao mingine | 20 Tsh/Dk |
| Kutuma SMS | 5 Tsh/SMS |
| Data (MB) | 9.35 Tsh/MB |

### GHARAMA ZA NJE YA NCHI

GHARAMA ZA KUPIGA SIMU NJE YA NCHI

| Kanda | Gharama (Tsh/Dk) |
|---|---|
| **Ukanda 1:** USA, UK, India, China, Canada, Australia, Japan, South Korea, Vietnam, Laos, Cambodia | 450 |
| **Ukanda 2:** Nchi nyingine za ULAYA, Kenya | 750 |
| **Ukanda 3:** Rwanda, Afrika Kusini, Zambia, UAE, Oman,Haiti, Peru | 840 |
| **Ukanda 4:** Cameroon, Zimbabwe, Malawi, Uganda, Congo DRC, Mozambique | 1,000 |
| **Ukanda 5:** Burundi | 1,350 |
| **Ukanda 6:** Sehemu nyingine duniani | 2,700 |
| **Ukanda 7:** Mitandao ya satelite | 13,800 |

GHARAMA ZA KUTUMA SMS NJE YA NCHI

| SMS | Gharama |
|---|---|
| SMS kwenda nje ya nchi | 95 Tsh/SMS |

### GHARAMA ZA VIFURUSHI

| Aina ya kifurushi | Muda | Gharama (Tsh) | Mitadao Yote (Dk) | Halotel-Halotel (Dk) | SMS | Data (MB) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| VIFURUSHI VYA SAUTI | | | | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 350 | 25 | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | | 110 | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | 60 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku | 1,000 | 180 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku 2 | 1,000 | 160 | | 25 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 1,500 | 180 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 2,500 | 350 | 50 | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 3,000 | 500 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 4,000 | 400 | 50 | 50 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 5,000 | 550 | 650 | 100 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 10,000 | 1,600 | 1,600 | 150 | |
| Dakika & SMS | Bila ukomo wa muda | 500 | 20 | | | |
| VIFURUSHI VYA SMS | | | | | | |
| SMS | Siku | 100 | | | 200 | |
| SMS | Wiki | 500 | | | 2000 | |
| SMS | Mwezi | 1,000 | | | 10,000 | |
| VIFURUSHI VYA INTANETI | | | | | | |
| Intaneti | Siku | 350 | | | | 170 |
| Intaneti | Siku | 500 | | | | 246 |
| Intaneti | Siku | 1,000 | | | | 492 |
| Intaneti | Siku | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Siku 10 | 2,100 | | | | 1,024 |
| Intaneti | Wiki | 1,000 | | | | 492 |
| Intaneti | Wiki | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Wiki | 3,000 | | | | 1,475 |
| Intaneti | Wiki | 5,000 | | | | 2,460 |
| Intaneti | Wiki | 10,000 | | | | 4,925 |
| Intaneti | Mwezi | 10,000 | | | | 4,920 |
| Intaneti | Mwezi | 20,000 | | | | 9,850 |
| Intaneti | Mwezi | 30,000 | | | | 14,780 |
| Intaneti | Miezi 2 | 50,000 | | | | 24,600 |
| Intaneti | Bila ukomo wa muda | 500 | | | | 200 |
| VIFURUSHI VYA COMBO | | | | | | |
| Combo | Siku | 500 | 15 | 10 | 5 | 200 |
| Combo | Siku | 1,000 | 60 | | 60 | 246 |
| Combo | Wiki | 2,000 | 55 | | 20 | 850 |
| Combo | Wiki | 2,500 | 20 | | 20 | 1,150 |
| Combo | Wiki | 3,000 | 100 | | 30 | 1,250 |
| Combo | Siku 10 | 3,100 | 150 | 20 | 300 | 1,024 |
| Combo | Mwezi | 10,000 | 280 | | 50 | 4,000 |
| Combo | Mwezi | 20,000 | 400 | | 100 | 8,500 |
| Combo | Mwezi | 50,000 | 600 | | 200 | 22,000 |

### GHARAMA ZA HUDUMA ZA ZIADA

- Hakuna makato yeyote kwa wateja wa Halotel kutumia huduma unganishi kwa njia ya USSD.
- Mteja wa Halotel atatumia huduma unganishi kwa njia ya SMS kwa Gharama kuanzia Shilingi 0 (Bure) hadi Tsh 100, kutegemeana na makubaliano ya kibiashara na mtoa huduma husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nishati safi mkombozi wa mazingira

**MIAKA** ya nyuma kabla ya kampeni ya matumizi ya nishati safi haijapamba moto, usafirishaji mkaa kutoka mikoani ulishamiri na uharibifu wa mazingira ulikuwa katika hali mbaya.

Kwa mifano michache kwa wanaopita Barabara ya Bagamoyo, ilikuwa huwezi kutembea bila kukutana na pikipiki au malori yaliyosheheni magunia ya mkaa.

Ukiangalia idadi ya magunia yaliyopakiwa kwenye malori hayo, utagundua ni jinsi gani misitu ilivyokuwa ikiangamia kwa kukatwa miti inayochomwa na kuwa mkaa.

Mbali na uharibifu wa mazingira, lakini matumizi ya kuni na mkaa yana athari kubwa katika afya za binadamu kutokana na moshi wanaouvuta.

Matumizi ya nishati safi ya gesi imesaidia kwa kiasi kikubwa kuepuka uchafuzi wa hewa ambao unasababisha uharibifu wa mazingira na pia kusababisha magonjwa mbalimbali.

Ulinzi wa afya ya mama, familia, mazingira na taifa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ni lazima uanzie jikoni.

Mkutano Mkuu wa Maboresho ya Serikali za Mitaa (TOA), ulieleza kuhusu tamanio la serikali kufikia asilimia 80 ya Watanzania wote kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2034.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa kinara wa kutangaza matumizi ya nishati safi ya kupikia na lazima taifa lianze sasa kubadilisha nishati inayotumiwa kupikia.

Mara kwa mara anapokuwa kwenye majukwaa mbalimbali ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, Rais anasema huwezi kumaliza au kupunguza ukataji miti unaoangamiza misitu kama hutaligusa jiko.

Kampeni ya Rais imefanya mengi, Watanzania wameelezwa umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kupikia zinazopunguza madhara kiafya, athari kwa mazingira na kijamii.

Na sasa Rais amelifikisha taifa kwenye kutekeleza Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034.

Analenga kaya zenye 'jiko safi na salama', ambayo asilimia 80 ya Watanzania watakuwa wanatumia jiko lenye nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Pamoja na kuwaondoa kinamama katika matumizi ya kuni na mkaa na kutumia nishati safi, pia taasisi kubwa ambazo zinahudumia watu wengi kupata chakula, zinahimizwa kuhama kwenye matumizi ya kuni na mkaa na kuhamia kwenye nishati safi ili kupunguza uharibifu wa hewa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, ili kufanikiwa katika matumizi ya nishati safi ipo haja ya kuwa uhamasishaji wa kutumia majiko yanayotumia nishati safi na yapatikane kwa urahisi ili wanayoyahitaji wasipate vikwazo kwa kuyapata.Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) inaeleza kuwa Tanzania Bara ina takribani kaya milioni 13.9.

Kufikia azma hiyo kaya zenye jiko safi na wakuu wa mikoa na wilaya wasimamie matumizi ya nishati safi ya kupikia na pia wizara na taasisi za umma kadhalika na sekta binafsi kuzingatia matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda mazingira na kuepusha athari nyingi zinazotokana na kutumia nishati zisizo safi.

Mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliagiza taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100, ifikapo Januari, mwaka huu, ziache kutumia kuni na mkaa kupikia.

Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mikakati yake inaeleza kuwa hilo limefanyika na taasisi nyingi zikiwamo za umma kuanzia Magereza, kambi za jeshi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vikuu vimeanza kutumia nishati safi ya kupikia.


Pia, juhudi zinafanywa na kila taasisi inayohusika na nishati na katika mbio za Mwenge wa Uhuru, mwaka huu, ujumbe mkubwa unaobebwa ni uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi kupikia.

Uhamasishaji huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuepusha athari zinazosababishwa na hewa chafu inayotokana na kuvuta moshi mchafu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Elimu zaidi dawa faini barabarani

Na Sabato Kasika

**KATIKA** kuhamasisha umma kutii sheria bila shuruti, polisi mkoani Mbeya kwa kushirikiana na taasisi zinazosimamia hakijinai za magereza na mahakama walianzisha kampeni.

Ililenga kuelimisha jamii kutambua umuhimu wa dhima hiyo ya kutii sheria bila kulazimishwa.

Elimu hiyo iligusa makundi mbalimbali wakiwamo madereva ili wanapoendesha vyombo vya moto wazingatie sheria za usalama barabarani badala ya kusubiri walazimishwe au washurutishwe.

Hata hivyo, pamoja na kampeni hiyo, bado utii wa sheria bila shuruti umekuwa ni changamoto mkoani humo na baadhi ya madereva huvunja sheria na kuendelea kusababisha makusanyo makubwa ya faini. Wingi huo wa makusanyo yanayotokana na makosa mbalimbali ya barabarani, unajidhihirisha katika taarifa ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya Benjamin Kuzaga anayoitoa hivi karibuni.

Kamanda Kuzaga anasema jeshi hilo limekusanya zaidi ya Sh. bilioni 3.4 kutokana na makosa mbalimbali ya ukiukwaji sheria za usalama barabarani katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2024.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la Sh. milioni 104.8 kulinganisha na mapato ya mwaka 2023 zilikokusanywa bilioni 3.3.

Niwapongeze polisi kwa mafanikio hayo, lakini nikija na ushauri kwamba, elimu kwa madereva inapaswa kupewa kipaumbele zaidi kuliko faini zinazotozwa kila uchao.

Uwapo wa makusanyo mengi ya fedha zinazotokana na faini za makosa mbalimbali, ni wazi kwamba kuna sehemu hapako sawa, hivyo ipo haja kwa jeshi hilo kujikita zaidi kwenye utoaji wa elimu kwa madereva. Ninaeleza hivyo, kwa sababu kila kukicha madereva wapya wanaingia barabarani ambao nao ni vyema wakapata elimu ya jinsi ya kutii sheria za usalama barabarani bila shuruti.

Ingawa inawezekana wapo baadhi ya madereva wasiotii sheria kwa makusudi, lakini njia hiyo inaweza kusaidia kupunguza wingi wa makusanyo hayo, yanayotangazwa. Wingi huo wa makusanyo ni dalili kwamba kuna sehemu hakujawa na mafanikio. Kupitia kampeni ya elimu ya kutii sheria bila shuruti, binafsi nilitarajia kupungua kwa faini kwani madereva wangetii sheria bila kulazimishwa.

Sio kwamba ninapinga kazi inayofanywa na jeshi hilo, ila ninalenga kujikita zaidi katika utoaji wa elimu ya usalama barabarani, kwani kila kukicha madereva wapya wanaingia barabarani.

Hivyo, elimu ikiendelea kutolewa kila wakati ili madereva wengi wawe wa zamani na wapya wataipate, wale ambao wataendelea kukaidi, watozwe faini zaidi, japo ni imani yangu kuwa elimu inaweza kupunguza faini.

Elimu hiyo inaweza kusaidia kutimiza moja ya malengo ya kampeni ya kutii sheria bila shuruti ambayo ni kuboresha maadili ya jamii kama msingi wa maendeleo yanayozingatia usalama, amani na utulivu ambavyo ni nguzo za ustawi wa kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Ikumbukwe kuwa msingi wa kampeni hiyo ulikuwa ni kuongeza ari na moyo wa uzalendo unaozingatia uwajibikaji katika harakati za kujiletea maendeleo bila kuvunja sheria za nchi.

Ninaamini madereva wakipewa elimu ya matumizi sahihi ya barabarani, itasaidia kupunguza ajali au makosa ambayo yanachangia kuwapo kwa ajali zinazokatisha maisha ya watu au kuwa na ulemavu wa kudumu.

Hivyo, njia bora ya kuwafanya madereva wawe na uelewa wa kutosha wa matumizi sahihi ya barabara, si kujikita kwenye makusanyo ya faini bali ingekuwa ni kuangalia chanzo cha makosa na kukifanyia kazi. Kimsingi elimu ni ya muhimu kwa maisha, katika shughuli za kila siku, awe mwanamke au mwanamume inampasa kupata elimu ili imsaidie kufanya maamuzi sahihi na kwa usahihi.

HABARI KITAIFA

# Mgomo wa madereva Lindi, Mtwara wamalizwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

MGOMO wa madereva wa mabasi madogo wanaohudumia abiria katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Lindi na Mtwara umeisha baada ya serikali kukubali hoja zao, zikiwamo za urejeshaji leseni za madereva wenzao kwa madai ya kusimamisha abiria ndani ya magari yao.

Madereva wanaohudumia wilaya za Masasi, Nanyumbu, Newala, Mtwara Mjini, Tandahimba mkoani Mtwara pamoja na Nachingwea, Ruangwa, Liwale, Mtama na Kilwa mkoani Lindi walisitisha huduma za kusafirisha abiria kutokana na wenzao wanane kunyang'anywa leseni kwa kosa la kusimamisha abiria. Kufuatia mgomo huo, viongozi na watendaji wa serikali, akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Victoria Mwamviva, walikutana na madereva hao kusikiliza hoja zao na kuzipatia ufumbuzi, ikiwamo kurejeshewa leseni zao.

Mbali na kurejeshewa leseni, madereva wa magari hayo pia wameruhusiwa kusimamisha abiria wasiozidi 15, wakiwamo watano kwa mabasi aina ya hiace na 10 kwa mabasi ya Coaster na TATA.

Wakizungumza baada ya kikao hicho kilichochukua zaidi ya saa nane, baadhi ya madereva hao, wakiwamo Maulidi Abdallah, Daudi Juma na Michael Joseph walipongeza serikali kukubali kusikiliza hoja zao na wako tayari kurejesha huduma za usafirishaji kwa wananchi.

Walishauri serikali iangalie upya kipengele cha usimamishaji abiria ndani ya mabasi yanayotoa huduma katika maeneo hayo ya Lindi na Mtwara, wakidai wanazingatia usalama tofauti na maeneo mengine nchini.

Baadhi ya abiria wanaohudumiwa na magari hayo walishukuru serikali kwa kukubaliana na madereva kwa kuwa katika kipindi cha mgomo wa madereva hao waliteseka vya kutosha, ikiwamo kulipa nauli kubwa kutoka kwa waendesha bodaboda.

Januari 8 mwaka huu, madereva wanane wa mabasi madogo walinyang'anywa leseni zao kwa tuhuma za kusimamisha abiria katika magari yao.

# Maofisa ununuzi 34 washushiwa kibano

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATAALAMU 34 wa ununuzi na ugavi wamechukuliwa hatua za kinidhamu baada ya kubainika kufanya uzembe ulioisababishia hasara serikalini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Godfred Mbanyi alieleza hayo juzi mkoani hapa wakati wa kikao cha wajumbe wa Bazara la Wafanyakazi la Bodi hiyo.

Kikao hicho kililenga kujadili na kupitia wasilisho la menejimenti kuhusu makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2025/26.

Mbanyi alisema bodi hiyo imekuwa inachukua hatua kali kwa wataalamu wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao, akibainisha kuwa hadi kufikia Desemba 2024, wataalam 34 kutoka maeneo mbalimbali nchini walikuwa wamechukuliwa hatua za kinidhamu.

> **"Kipindi cha nyuma bodi ilikuwa ikipata changamoto nyingi, lakini kwa sasa hata kesi mbalimbali kutoka kwa viongozi wetu wakuu walizokuwa wakiziibua...**

Alisema kutokana na hatua hiyo bodi kwa sasa inajuvunia wataalam wake kuanza kuelewa ya kwamba serikali na taifa inawategemea kwenye mchakato wa manunuzi yenye kufuata sheria, taratibu na maadili.

"Kipindi cha nyuma bodi ilikuwa ikipata changamoto nyingi, lakini kwa sasa hata kesi mbalimbali kutoka kwa viongozi wetu wakuu walizokuwa wakiziibua wakiwa wanafanya ziara zimepungua," alisema Mbanyi.

Alisema kila mwaka bodi inachukua hatua kwa wataalamu wanaokiuka utaratibu na kwa sasa wamenza kuogopa na kufanya kazi kwa uaminifu.

"Iwapo mradi unajengwa ni daraja, shule au kituo cha afya ni mali ya Watanzania na mtaalamu anapofanya uzembe, sisi bodi tunashughulika naye, hatuangalii mtu kala rushwa bali tunaangalia kwamba hukutekeleza wajibu wake," alisema.

Kadhalika, alisema bodi imeboresha mfumo yake ya usajili wenye kutambua namba za usajili ambao umeunganishwa na mfumo wa ununuzi wa umma.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi, Shilla Mwandu alishukuru serikali kwa utaratibu nzuri ambao wameweka ikiwamo kuanzisha mabaraza ya vyama vya wafanyakazi katika taasisi zake.




# Tanzania imejipanga kupokea wakuu wa nchi 53 Afrika mkutano nishati

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Nishati anayeshughulikia umeme na nishati jadidifu, Dk. Khatibu Kazungu amesema, Tanzania imejipanga vema kupokea ugeni wa wakuu wa nchi 53 wa Afrika watakaohudhuria mkutano wa wakuu wa nchi wa masuala ya nishati unaotarajiwa kufanyika Januari 27 na 28, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Dk. Kazungu aliyasema hayo kwenye mkutano wa Baraza la 15 la Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (IRENA) wakati akiwasilisha mada kwenye mjadala wa ngazi ya juu wa mawaziri wenye lengo la kujadili namna nchi wanachama watatumia fursa ya ushawishi kwa wadau wa maendeleo kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya nishati jadidifu ambayo ni rafiki kwa mazingira.

"Nipende kuwajulisha kuwa Tanzania ni mwenyeji wa mkutano huo wa masuala ya nishati na ajenda hii kama nchi tumeibeba kwa vitendo kuhakikisha Waafrika milioni 300 kusini mwa Jangwa la Sahara wanapata umeme ifikapo mwaka 2030 na natoa rai kwa nchi wanachama wa IRENA kuibeba ajenda hii kwa vitendo," alisema Dk. Kazungu.

Alisema mkutano wa M300 utaangazia pia mageuzi kwenye sekta ya nishati na kuangalia uwezekano wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuunganisha wateja na ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye utekelezaji wa miradi ya pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Dk. Kazungu aliwaambia wajumbe wa IRENA kuwa kaulimbiu itakayoongoza mkutano huo ni kuharakisha upatikanaji wa nishati Afrika ili kuwatoa gizani waafrika wapatao milioni 685 kati ya bilioni moja ambao hawana nishati ya umeme.

Alisema serikali ya Tanzania imefanya marekebisho ya sheria ya uwekezaji ili kutoa fursa kwa sekta binafsi kushirikiana na serikali kutekeleza miradi ya nishati jadidifu kutokana na umuhimu wake.

Alisema Tanzania inawashukuru wabia wa maendeleo kwenye utekelezaji wa miradi ya nishati jadidifu ikiwamo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), AFD, KFW kwa kufadhili miradi mbalimbali ya nishati jadidifu nchini ikiwamo ya Kakono na Malagarasi ambayo iko kwenye hatua za utekelezaji.

Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Nishati na Mabadiliko ya Tabianchi kutoka Benki ya AfDB, ambao pia wanafadhili miradi ya nishati jadidifu kwa upande wa Afrika, Kevin Kariuki, alisema kuwa utashi wa kisiasa, uainishaji wa sera za wazi vinahitajika kwenye utekelezaji wa miradi ya umeme kwa nchi za Afrika ili iweze kuleta tija kwa wananchi wake.

Alisema ni wakati kwa nchi za Afrika kuchangamkia fursa za utekelezaji wa miradi ya nishati ambayo ni rafiki kwa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza hewa ya ukaa na kuzitaka jumuiya za kimataifa kuunga mkono azimio hilo kwa vitendo.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, akiwapigia magoti wananchi wa vijiji vya Msikii na Munkhola ikiwa ni msisitizo wa kuwaomba waondoke katika eneo walilovamia la Hifadhi ya Msitu wa Munkhola, Wilaya ya Hanang mkoani Manyara jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Bibi aliyetelekezewa pacha, aomba msaada

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Kata ya Mwendakulima, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Kashindye Mhoja (64), anaomba msaada wa kuwalea wajukuu zake pacha wa mwezi mmoja baada ya mkwewe kuwatelekeza.

Alisimulia kuwa tukio hilo lilitokea Oktoba 27 mwaka jana baada ya kutoka kwenye maziko ya mama wa watoto hao ambaye ni binti yake yaliyofanyika kata ya Ulowa, Halmashauri ya Ushetu.

Alisema mkwewe huyo bila kujali umri wake alimtelekezea pacha hao kisha kutokomea.

Kashindye, alisema kabla ya mkasa wa kufiwa na binti yake alitoweka nyumbani kwake na kwenda kusikojulikana na kurudi na ujauzito wa watoto hao kutokana na kusumbuliwa na tatizo la upungufu wa damu mara kwa mara.

Alisema alijifungua salama watoto hao katika Kituo cha Afya cha Mwendakulima.

"Baada ya kujifungua akaendelea kuwalea watoto wake, Oktoba 25 niliitwa na jirani na kuniambia binti yangu amezidiwa ndani na nilipofika nilikuta amefariki dunia, nikatoa taarifa kwa viongozi wa mtaa," alisema Kashindye.

Alisema baada ya maziko, Oktoba 27 na kurejea nyumbani, siku mbili baadaye mkwewe akatokomea kusikojulikana na kutelekeza pacha hao.

Alisema familia yake haifahamu nyumbani kwa mkwewe japo walikuwa wakisikia akijitambulisha kuwa ni mzaliwa wa Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu.

Kwa mujibu wa bibi huyo, anaishi na wajukuu zake hao katika mazingira magumu kwa kukosa mahitaji.

Alisema wanalala chini kwa kutandika maboksi na sandarusi huku afya zao zikiendelea kudhoofika na kuomba msaada pia wa kumtafuta baba wa watoto.

Kashindye aliwaomba wadau wa maendeleo ikiwamo vituo vya kulelea watoto yatima kumuunga mkono katika malezi ya wajukuu hao hasa katika upatikanaji wa maziwa na mahitaji mengine ili wapate makuzi na malezi kutokana na hali zao kudhoofu kwa kukosa lishe.

Mmoja wa majirani wa bibi huyo, Henery Masolwa, alisema familia hiyo inapitia kipindi kigumu katika malezi ya watoto licha ya jamii kushirikiana nayo kwa kuwachangia baadhi ya vitu yakiwamo mavazi na vyakula.

# DC awapigia magoti wananchi, awaomba waondoke hifadhini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe amewapigia magoti wakazi wa vijiji vya Msikii na Munkhola, akiwaomba waondoke ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Munkhola baada ya kudaiwa kuvamia kwa kilimo na ujenzi wa makazi.

Eneo hilo kwa sasa limeanza kupata mmomonyoko wa ardhi unaoweza kusababisha madhara na wakazi wa vijiji hivyo wanadaiwa kuvamia na kujimilikisha kinyume na sheria na kufanya shughuli zao.

Shughuli hizo ni pamoja na kilimo na ujenzi wa makazi ambao umesababisha mmomonyoko wa ardhi kuharibu nyumba zaidi ya 150.

Gondwe alifika katika eneo hilo juzi akiongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na kushuhudia uharibifu huo, hali iliyomlazimu kupiga magoti kama msisitizo wa kuwasihi wakazi hao kuondoka katika hifadhi hiyo.

Akizungumza na wakazi wa vijiji hivyo, Gondwe alitoa muda wa miezi mitatu kwa wananchi wanaojihusisha na shughuli hizo kuondoka ndani ya hifadhi hiyo.

"Nisikilize hatutanii, nawapa miezi mitatu muwe mmeshaondoka kwenye hifadhi," alisema Gondwe.


Alisema kutokana na uharibifu unaofanyika ndani ya msitu huo kuna maporomoko yanapeleka maji ndani ya Kijiji cha Munkhola na kusababisha vyoo kutitia, huku nyumba zikijaa maji na kuhatarisha maisha ya watu.

Aliwataka wakazi hao kutambua kuwa wana wajibu wa kutunza hifadhi kwa manufaa ya vizazi vyao na kwamba kuharibu hifadhi ni ubinafsi.

Alisema wananchi waliouziwa ardhi katika eneo hilo wametapeliwa kwa sababu wenye mamlaka ya kufanya hivyo ni mkutano mkuu wa kijiji na wajumbe ni wananchi na siyo Halmashauri Kuu ya Kijiji.

"Kama uliuziwa ardhi na Halmashauri ya Kijiji na kijiji kinasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya wamekutapeli kachukue hela yako, ardhi ya kijiji sio mali ya Halmashauri ya Kijiji," alisema Gondwe.

Baadhi ya wakazi wa eneo hilo walisema hali ni mbaya katika vijiji vyao kutokana na maji kujaa na vyoo kutitia kwa sababu ya uharibifu wa msitu huo.



# Wataalam wa anga duniani kukutana Arusha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATAALAMU wa viwanja vya ndege wapatao 300 duniani wanatarajia kukutana jijini hapa Aprili mwaka huu kujadili maendeleo endelevu sekta ya anga.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Waziri wa Uchukuzi Profesa Makame Mbarawa, alisema Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa 73 wa Baraza la Kimataifa la Viwanja vya Ndege Kanda ya Afrika (ACI), utakaowakutanisha wataalamu hao ndani na nje ya Bara la Afrika.

Prof. Mbarawa, alisema wizara yake kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) inaendelea na maandalizi ya mkutano huo utakaoanza Aprili 24 hadi 30 mwaka huu na kuhudhuriwa na wajumbe hao kutoka nchi 54 za Afrika na nje ya bara hilo, yakiwemo mashirika 59 ya biashara yanayoendesha viwanja vya ndege 265.

Kauli mbiu ya mkutano huo ni "Katika kuelekea wakati ujao bora wa kijani kutumia usafiri wa anga endelevu na utalii kwa ustawi wa kiuchumi".

Waziri huyo alifafanua kuwa lengo la mkutano huo ni kuhakikisha kunakuwepo na uendelevu, usalama na ufanisi katika usafiri wa anga na uzingatiaji wa mazingira.

Tukio hilo litaangazia maendeleo endelevu katika sekta ya usafiri wa anga na kuonesha dhamira ya Tanzania katika utunzaji wa mazingira.

Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Abdul Mombokaleo, alisema menejimenti yao imejipanga kuhakikisha inaimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika viwanja vyote vya ndege na miradi ya kibiashara ikiwemo hati miliki.

Alisema mkutano huo kutokana na umuhimu wa sekta hiyo unafanyika jijini Arusha na Tanzania kupata fursa ya kujitangaza na vivutio vyake vya utalii.

# Msithubutu kuchagua watoa rushwa, kanisa laonya

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MAKAMU Mkuu wa Askofu wa Kanisa la Kilutheri Afrika Mashariki (KKAM), Dk. Philemon Langasi amewaonya Watanzania wasithubutu kuchagua viongozi wanaotoa rushwa katika Uchaguzi Mkuu nchini mwaka huu ili taifa lipate maendeleo.

Dk. Langasi alitoa kauli hiyo jana katika Mtaa wa Uzunguni kwa Wasomali, Parokia ya Semento ya Jimbo la Hai la Dayosisi ya Arusha ya KKAM wakati wa ibada maalum ya kuweka wakfu eneo la ibada, kumbariki Mtheolojia Eneza Kitange kuwa Mchungaji na wazee wa kanisa hilo.

Alionya kuwa viongozi wanaoingia madarakani kwa kutoa fedha, wanajali maslahi yao zaidi badala ya umma na kuwawajibisha ni kazi ngumu.

Aliwataka Watanzania kumuomba Mungu kupata kiongozi anayefaa kuwaongoza.

"Namuomba mama Samia (Rais Samia Suluhu Hassan), ambaye katika kipindi chake ameongoza vizuri sana aweke ile mifumo ikae sawa sawa ili haki iweze kutendeka. Ninachoamini bado Watanzania wanampenda kwa kazi nzuri alizofanya na watamchagua," alisema Langasi ambaye pia ni Askofu Mkuu wa Dayosisi ya Arusha ya Kanisa hilo.

"Nina wito pia kwa mwaka huu wa 2025, ambao wote kama tunavyojua ni wa uchaguzi katika nchi yetu ya Tanzania. Ni mwaka ambao unagubikwa na matukio ya ajali zisizo na mfano, watu kutekwa, uharibifu wa kila aina na hata wengine wakiyapa majina," aliongeza.

> **"Nina wito pia kwa mwaka huu wa 2025, ambao wote kama tunavyojua ni wa uchaguzi katika nchi yetu ya Tanzania. Ni mwaka ambao unagubikwa na matukio ya ajali...**

Askofu mwingine wa kanisa hilo, Dk. Philemon Mollel (Monaban), alikemea viashiria vya uvunjifu wa amani katika uchaguzi ujao na kusisitiza kuwa malalamiko madogo yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji mwaka 2024 hayapaswi kujirudia.

Baada ya Mtheolojia Kitange, kubarikiwa kuwa Mchungaji mpya wa KKAM, alisema Watanzania wanahitaji kuishi kwa amani na wanamuomba Mungu uchaguzi mkuu ujao wa rais, wabunge na madiwani ufanyike kwa uhuru na haki.

"Tufanye uchaguzi bila uvunjifu wa amani, tufanye uchaguzi kwa kumtumainia Mungu kwa kuwa bila kuwa na amani, taifa la Mungu litaangamia. Hatuwezi kuishi maisha ya kumpendeza Mungu kama taifa halina amani,"alisema Kitange.

Aliwataka wananchi, wasimamizi wa uchaguzi, wapiga debe na watia nia, kuingia kwenye maombi ya kweli ili taifa liwe na amani kwa wakati huo na baada ya hapo.



Rachel Mkindi mwalimu wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Mwambao wilayani Muheza, mkoani Tanga, akiwafundisha wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Viwanda kutoa ajira milioni 6.4 nchini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WIZARA ya Viwanda na Biashara imetangaza mpango wake wa kukuza uchumi nchini kwa kuanzisha viwanda zaidi ya 9,048 vyenye uwezo wa kutoa ajira milioni 6.4 kwa kipindi cha miaka mitano ijayo

Mpango huo ulitangazwa mwishoni mwa wiki jijini hapa na Waziri wake, Dk. Selemani Jafo wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha wakurugenzi na wakuu wa taasisi zilizopo chini ya wizara hiyo kujadili bajeti na vipaumbele vyake kwa mwaka wa fedha wa 2024/25.

Ili kufanikisha mpango huo kuanzia mwaka huu hadi 2030, Jafo, aliwaagiza wakurugenzi na wakuu hao kuwashirikisha makatibu tawala na wakuu wa mikoa kushiriki uzinduzi wa tathmini hiyo.

Vilevile, aliagiza kila mkoa kufungua viwanda vidogo na vya kati ili kuchochea ajira kwa wahitimu wa vyuo na shule.

Jafo, pia aliagiza taasisi hizo kupambana na bidhaa feki kwa kuwa zinaathiri uwekezaji wa viwanda vya ndani na kuharibu masoko nje ya nchi.

Kwa upande waTaasisi ya Zana za Kilimo, aliagiza kuendelea kufanya utafiti ili kuleta matokeo chanya ya teknolojia.

Alisema bajeti hiyo ndio itatoa taswira nzuri ya utekelezaji wa majukumu ya wizara hiyo na uwezeshwaji wa ufanisi zaidi.

Aliwataka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kuongeza kasi zaidi utoaji leseni kwa njia ya mtandao na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kudhibiti magendo nchini hususani maeneo ya mipaka ya Tanzania na nchi za nje.

Akizungumzia kuhusu mpango wa serikali wa stakabadhi ghalani, Jafo, alisema umepelekea kupanda kwa bei ya zao la mbaazi kutoka Sh.1,600 hadi kufikia Sh.2,200 katika baadhi ya mikoa ukiwamo wa Lindi na kuzaa matunda.

Awali Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hashil Abdallah, alisema kikao hicho kina lengo la kupanga mikakati na vipaumbele kwa mwaka 2024/2025 na utekelezaji wa vipaumbele vyake.





# Wajasiriamali waitwa kukopa mamilioni ya fedha

**Na Halima Ikunji,**
TABORA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora imepokea Sh. milioni 100 zilizotolewa na serikali kutoa mikopo yenye riba nafuu na kuwahamasisha wafanyabiashara wadogo kuchangia na kuinua kipato.

Ni baada ya serikali kurejesha utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali nchini na kuzinduliwa Oktoba 17, mwaka jana jijini Arusha na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Doroth Gwajima.

Akitoa taarifa juzi wakati wa ziara ya Dk. Gawajima, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, John Tesha, alisema wamesajili wafanyabiashara 85 na kuwapatia vitambulisho vya kidijiti kama ilivyoelekezwa na Serikali.

Tesha, alisema vitambulisho hivyo vitawawezesha kuomba na kupata mikopo hiyo muhimu kuwainua kiuchumi wajasiriamali hao wadogo wilayani hapa. "Tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha mfuko huu maalumu kwa ajili ya kuwezesha wafanyabiashara wadogo wa kike na kiume mikopo nafuu itakayochochea shughuli zao na kuirejesha taratibu na riba kidogo tu," alisema.

**Tesha alisema wilaya hiyo ina wafanyabiashara 688 na hamasa ya kuwasajili kidijiti inaendelea kwa kuingizwa katika mpango huo ili kunufaika na mikopo...**

Tesha alisema wilaya hiyo ina wafanyabiashara 688 na hamasa ya kuwasajili kidijiti inaendelea kwa kuingizwa katika mpango huo ili kunufaika na mikopo hiyo.

Alisema katika mwaka wa fedha 2024/25, halmashauri hiyo ilitenga Sh.milioni 750 za mapato ya ndani kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu ili kuwakwamua kiuchumi.

"Sh.milioni 107 zimetolewa kwa baadhi ya vikundi mwezi Oktoba 2024 na mpango ya kutoa mikopo zaidi kwa vikundi vingine inaendelea, hivyo tunawakumbusha wananchi zaidi kujiunga katika vikundi ili wanufaike na mikopo hiyo," alisema Tesha. Kwa upande wake, Waziri Gwajima, alisema serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 10.5 nchi nzima kwa ajili ya kuwawezesha wafanyabiashara wa kike na kiume kupata mikopo yenye riba nafuu na kuwaomba kuchangamkia fursa hiyo.

Wakati huo huo; Dk. Gwajima amekabidhi mashine ya kulimia yenye thamani ya Sh.milioni 30 iliyotolewa na Halmashauri hiyo kama mkopo usio na riba kwa Kikundi cha Wanawake wa Mwendokasi na kuwataka kuitumia kujiinua kiuchumi.



Katibu Tawala Msaidizi (Miundombinu) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Chagu Ng'oma (aliyesimama kulia), akizungumza na timu ya mkandarasi M/S Dimetoclasa Real Hope Limited anayetekeleza mradi wa ujenzi wa hospitali ya rufani yenye hadhi ya mkoa wilayani Ukerewe pamoja baadhi ya watumishi kutoka Idara ya Afya Mkoa wakati wa ukaguzi wa utekelezaji wa mradi huo, ulioanza hivi karibuni. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Shule kugawanywa kwa msongamano

**Na Ambrose Wantaigwa,**
TARIME

HALMASHAURI ya Wilaya ya Tarime mkoani Mara inatarajiwa kuigawa Shule ya Msingi Muriba na kuanzisha nyingine kukabiliana na msongamano wa wanafunzi darasani ili kuinua kiwango cha elimu.

Hayo yalielezwa juzi na Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri hiyo, Alfred Magori wakati wa ziara ya Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara kukagua ujenzi wa madarasa jimboni humo.

Magori, alisema hatua hiyo inatokana na malalamiko kutoka kwa wazazi kuwa wanafunzi zaidi ya 100 wanasoma katika darasa moja kinyume na utaratibu wa Wizara ya Elimu kuwa na wasiozidi 45.

Alisema wataalam wa elimu wanakamilisha maandalizi ya awali ikiwemo miundombinu ya utawala na kitaaluma ili kuokoa wanafunzi hao zaidi 1,200 wanaolazimika kukusanywa eneo moja.

Waitara aliwataka wananchi waendelee kuchangia ujenzi wa miundombinu ya umma na kukataa kukatishwa tamaa na watu wasio na nia njema kwa maendeleo yao.

Alipongeza hatua ya wazazi wa wanafunzi hao kushirikiana na wananchi kukusanya vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kuongeza madarasa katika shule hiyo.

"Tunawaomba wazazi na wananchi warudi wakae chini na uongozi wa shule wakubaliane namna bora ya kuchangia kutatua msongamano wa wanafunzi chini ya usimamizi wa wataalam kutoka halmashauri, " alisema mbunge huyo.

Alisema anaunga mkono mikakati ya mwanzo kukabiliana na msongamano shuleni hapo na halmashauri ya wilaya hiyo kuanzisha awamu mbili za masomo kila siku.

# Wanafunzi 'gheto' waacha masomo kwa mimba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya wanafunzi wa kike wanaoishi kwenye vyumba walivyopanga jirani na Shule ya Sekondari ya Chona iliyopo Halmashauri ya Ushetu wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, wameacha masomo baada ya kupata mimba, imeelezwa.

Hayo yalithibitishwa na Mkuu wa Sekondari hiyo, Mwalimu Lucy Kibela katika mahojiano na Nipashe baada ya harambee ya kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike shuleni hapo.

Mwalimu Lucy, alisema wanafunzi hao wanaoishi kwenye vyumba hivyo maarufu kama gheto, wamekuwa wakirubuniwa na wanaume kwa kupewa chakula na fedha za matumizi madogomadogo kutokana na umasikini.

Lucy, alisema wanaume hao wamekuwa wakishawishi wanafunzi hao wa kike kwa kuwapa vyakula na fedha kama chambo ya kuwanasa na kufanya nao mapenzi kisha kupata ujauzito, kutelekezwa na kuacha masomo.

Alisema kwa mwaka jana, kati ya wanafunzi 241 wa kidato cha kwanza 71 wameacha masomo na kutokomea kusikojulikana, wengi wao wakiwa wa kike. Alisema vitendo hivyo vimekuwa vikiikumba shule hiyo licha ya kutoa elimu ya madhara ya ndoa na mimba za utotoni kwa wanafunzi wa kike na jamii ili watimize ndoto za kupata elimu.

Alisema hali hiyo imekuwa ikitokea mara kwa mara katika kipindi cha mavuno ambacho wanafunzi hao wanarubuniwa kwa vyakula na pesa baada ya wakulima kuuza mazao. "Tangu nimepangiwa sekondari hii kuwa mwalimu mkuu mwaka 2020 mpaka sasa wanafunzi 20 wamepewa mimba, kubakwa na vijana kwenye magheto na kuacha shule. 2024 wanafunzi watatu wameacha masomo kwa kupata mimba pia," alisema Lucy. Alisema tatizo hilo ni kubwa hivyo linahitaji kupatiwa ufumbuzi kwa wanafunzi hao wa kike kujengewa bweni shuleni na kuwekewa ulinzi kuwadhibiti kwenda kuzurura mitaani.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chona, Masamaki Madaha, alithibitisha baadhi ya wanafunzi kukatisha masomo kwa kupewa ujauzito kwa kuishi kwenye 'gheto' na kutembea umbali mrefu.

Madaha, alisema wanashirikiana na askari wa jadi 'sungusungu' kukabiliana na hali hiyo ili kuhakikisha wanafunzi wote wanahitimu masomo yao vema.

Alisema wanafunzi wengi wamepanga 'gheto' mitaani kutokana na kutoka vijiji vya mbali vya Busenda, Itebele, Ishila, Nhimbo, Nsalaba na Nshimba.

Diwani wa Kata hiyo, Mabala Mlolwa alisema kwa kushirikisha vijiji hivyo saba na vitongoji vyake, wamehamasisha kila kijiji kuchangia malori matano ya mawe na kitongoji mifuko mitatu ya saruji na kuanza ujenzi wa bweni hilo kukabiliana na ndoa na mimba za utotoni kwa wanafunzi.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani aliwakanya vijana kuacha kujihusisha kwenye mapenzi na wanafunzi kwani ni kinyume na sheria na kwamba hatua kali zitachukuliwa kwa watakaokaidi amri hiyo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 14, 2025
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Moto usiojulikana chanzo unavyoitikisa Marekani


Ukurasa 14

Zingatia haya kuandaa watoto kukurithi iwapo utatwaliwa


Ukurasa 13

Kupata kiu ya sekondari nyingi za sayansi, kwa wagusa wananchi

ELIMU

NA RESTUTA JAMES

SIGARA NI KITANZI

# Watafiti wanakupakulia mapya, ukivuta tatu umekata saa moja ya umri wako

• Paketi inamaliza saa 7 za maisha pigeni hesabu mmezivuta ngapi

WAKATI madaktari bingwa wa magonjwa yasiyoambukizwa wakionya kuhusu athari za matumizi ya tumbaku, utafiti mpya umebaini kwamba sigara moja inayovutwa, inapunguza dakika 20 za maisha ya anayevuta.

Aidha, wanawake wanapoteza dakika 22 za kuishi kwa kila sigara moja wanayovuta, wakati wanaume wanapoteza umri huo kwa dakika 17.

Maradhi yasiyoambukiza ni pamoja na saratani, mfumo wa hewa, kisukari na shinikizo la juu la damu na figo.

Utafiti huo umechapishwa kwenye jarida la Addiction hivi karibuni unaonesha kwamba kama mtu anavuta pakiti ya sigara 20 kwa siku, anapoteza karibu saa saba za maisha kwa kila pakiti.

Mtafiti Mkuu na Mwandishi Mkuu wa Utafiti huo, Dk. Sarah Jackson, anasema uamuzi wa kuacha sigara na aina yoyote ya tumbaku ni muafaka ili kuokoa uhai na kupunguza mzigo wa magonjwa yanayozuilika.

Dk. Sarah anasema kwenye utafiti huo kwamba wakati watumiaji wa tumbaku wanapoteza umri wa kuishi, wanaongeza mzigo kwa wapendwa wao ambao watalazimika kuwauguza wanapopata maradhi ya saratani, kisukari, shinikizo la damu na athari za mfumo wa hewa.



Kuvuta sigara kunatajwa kuwa ni kama kujinyonga kwa sababu muda wote inapunguza maisha. **PICHA:MTANDAO**

"Hii ni kwa sababu katika kipindi cha baadaye cha maisha yako watumiaji wa tumbaku huelekea kuishi katika afya mbaya zaidi," anaonya.

Utafiti huo, ambao umeidhinishwa na Idara ya Afya ya Jamii ya Uingereza, unajumuisha takwimu za vifo zilizotolewa na utafiti wa madaktari wa Uingereza ambao ulionyesha kuwa kwa wastani, watu waliovuta sigara katika maisha yao yote wanapoteza karibu miaka 10 ya maisha ikilinganishwa na watu ambao hawakuvuta sigara.

Wakati takwimu zikiwa hivyo Uingereza, huko Marekani hali ni hiyo hiyo kwani watumiaji wa tumbaku wanapunguza umri wa kuishi kwa miaka 10 ikilinganishwa na wasioitumia, kwa mujibu wa Vituo vya Marekani vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa.

Kwa ujumla, utafiti huo wa Uingereza unaonyesha kuwa madhara yanayosababishwa na matumizi ya tumbaku ni mengi na mabaya.

Hata hivyo, Dk. Sarah anasema pamoja na kwamba ni vigumu kurejesha umri ambao umeshapotea, anashauri watumiaji waache.

"Tafiti zimeonyesha kuwa watu ambao waliacha wakiwa na umri mdogo kwenye miaka 20-30, wana kuwa umri wa kuishi sawa na watu ambao hawajawahi kuvuta sigara.

Lakini kadiri unavyozeeka, hatua kwa hatua unapoteza zaidi umri wako, lakini hata uwe na umri gani unapoacha, sikuzote utakuwa na muda mrefu wa kuishi kuliko kama ungeendelea kuvuta sigara.

Kwa hiyo, kwa kweli, ingawa hubadili maisha yaliyopotea tayari, unazuia upotevu zaidi wa muda wa kuishi."

Katika utafiti huo, Dk. Sarah na wenzake, wanaeleza kuwa kwa mtu aliyekuwa anavuta sigara 10 kwa siku ambaye ameacha kutumia kwa siku nane, anaweza kurejesha siku moja ya maisha yake iliyokuwa imepotea.

"Kama umeacha tangu Januari Mosi, kufikia Februari 08, mwaka huu, unaweza kurejesha umri wa kuishi kwa wiki nzima na mwezi mzima kufikia Agosti 05, mwaka huu kama utaacha kwa mwaka huu wote, utajirejeshea siku 50," anasema.

"Kuacha kuvuta sigara na matumizi yote ya tumbaku ni jambo bora zaidi unaweza kulifanya kwa ajili ya afya yako. Mara tu unapoacha kuvuta sigara utaishi muda mrefu," anasema Dk. Sarah.

Aidha, ingawa viwango vya uvutaji sigara vimekuwa vikipungua tangu miaka ya 1960, matumizi ya tumbaku yanatajwa kuwa sababu kuu ya magonjwa na vifo vinavyoweza kuzuilika. Mathalani, nchini Marekani matumizi ya tumbaku huua zaidi ya Wamarekani 480,000 kila mwaka.

Utafiti tofauti, uliochapishwa mwaka jana katika jarida la Nature, uligundua kuwa uvutaji sigara unaweza kuwa na athari za muda mfupi na za muda mrefu kwenye mfumo wa kinga ya mtu, na kuwaacha katika hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa kama saratani.

Mwandishi mwenza wa utafiti huo, Dk. Darragh Duffy, anasema wavuta sigara walioacha walionesha hatua moja ya mabadiliko katika mfumo wa kinga.

"Habari njema ni kwamba, walau kuna mabadiliko kwenye kinga. Si wakati mzuri wa kuanza kuvuta sigara, lakini ikiwa wewe ni mvutaji sigara, wakati mzuri wa kuacha ni sasa," anasema.

Wakati utafiti ukibaini namna matumizi ya tumbaku yanavyopunguza umri wa kuishi, watengenezaji wa bidhaa hizo wameongeza vionjo vya ladha

**INAENDELEA UK.12**

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Moto usiojulikana chanzo unavyoitikisa Marekani

## • Kuliangamiza jiji la pili kwa ukubwa

MOTO asilia au wa nyika usiozimika ama mgumu kudhibitika unateketeza sehemu kadhaa za jiji la Los Angeles kwenye jimbo la California nchini Marekani.

Umesababisha vifo vya takriban watu 16, kuharibu mamia ya majumba, miundombinu na kulazimisha zaidi ya wakazi 130,000 kukimbia nyumba zao za kifahari katika jiji hilo la pili kwa ukubwa Marekani.

Licha ya jitihada za wazima moto, miale mikubwa ya moto inaelezwa kuwa inaendelea kushika kasi, huku hali ya hewa ya ukame na ukavu na athari za mabadiliko ya tabianchi zikitarajiwa kuendelea kuzidisha moto kama huo siku zijazo.

Kwa mujibu wa taarifa za CNN, watu 16 wamefariki wakati nyumba 5,000 zimeharibiwa na moto huo ambao unatajwa kuwa haujawahi kuonekana katika jimbo hilo la California.

**NI NINI SABABU?**

Watu wanaweza kujiuliza inakuwaje kuwe na moto wa asili ambao hakuna anayehusika kuuwasha?

Kwa mujibu wa taarifa za kimtandao, unaweza kuwashwa na radi, inauwasha kwa kutoa moto unaoshika mimea na vitu vikavu na kuviunguza.

Radi inatoa joto la kutosha kuwasha moto miti na chochote kikavu ambacho kinaweza kuungua na kuwa moja ya vyanzo vya moto asilia.

Milipuko ya volkano inatajwa kuwa ni chanzo pia, Lava ya moto au uji mzito au mwepesi kutoka ndani ya miamba chini ya ardhi inaweza pia kusababisha moto. Unaposhika vitu vikavu huviwasha.

Kadhalika mlipuko wa volkano unoambatana na cheche na moto unawasha moto eneo jirani kwa kuunguza vitu vikavu au chochote kinachoweza kushika moto.

Lakini, katika hali ya joto, hasa katika maeneo yenye ukavu mfano jangwani, mbuga au nyika kulikojaa mimea na vitu vingi vikavu na hewa nyingi ya kaboni, moto wa asili unaweza kuzuka moja kwa moja na kuteteza misitu, nyumba miundombinu na kukatisha maisha ya viumbe hai.

Kwa kurejea moto unaowaka Marekani kwenye jiji la pili kwa ukubwa la Los Angeles, BBC inasema maofisa wanataja upepo mkali na ukame katika eneo hili, umeifanya mimea kuwa mikavu na rahisi kuwaka moto, lakini pia athari za



mabadiliko ya tabianchi zinatajwa.

Hata hivyo, ingawa mazingira halisi bado hayajulikana, inaelezwa kuwa zaidi ya asilimia 95 ya matukio ya moto katika eneo hilo inaanzishwa na binadamu, kulingana na David Acuna, mkuu wa kikosi cha moto cha California.

Ingawa maofisa hawajatoa maelezo kamili kuhusu chanzo cha moto huu wa sasa, kipengele muhimu kilichotajwa katika kuenea kwa moto huo ni upepo wa Santa Ana, ambao unapuliza kutoka bara kuelekea pwani.

Unasafiri kwa kasi ya zaidi ya maili 60 kwa saa sawa na kilometa 97 kwa saa, inaaminika kuwa upepo huo umekuwa ukifanya moto kuzidi kuwaka na kuteketeza kazi zote zilizofanywa na binadamu.

Mabadiliko ya tabia nchi yamechangia, ingawa upepo mkali na ukosefu wa mvua vinachochea moto, wataalamu wanasema kuwa mabadiliko hayo yanabadilisha hali ya kawaida na kuongeza uwezekano wa milipuko kama hiyo ya moto kwa miaka mingi ijayo.

Utafiti wa serikali ya Marekani hauna shaka katika kuhusisha mabadiliko ya tabianchi na milipuko mikubwa na kali ya moto upande wa magharibi wa nchi hiyo, inasema BBC.

"Mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo joto kali, ukame mrefu, na anga linayohitaji mvua, imekuwa kichocheo katika kuongezeka kwa hatari na ukubwa wa moto katika eneo hilo," inasema Idara ya Kitaifa ya Oceanic na Hali ya Hewa.

Baada ya msimu wa joto kali na ukosefu wa mvua katika miezi ya karibuni, California iko katika hatari kubwa, msimu wa moto kusini mwa California kawaida huaminika kuanza Mei hadi Oktoba, lakini Gavana wa jimbo hilo, Gavin Newsom, anaeleza mapema kuwa milipuko ya moto imekuwa tatizo la kila mwaka.

"Hakuna msimu wa moto," anasema ni mwaka wa moto."

Akizungumza na BBC, Acuna anasema kuwa moto wa Palisades unatokea mara ya tatu katika miaka 30 iliyopita ambapo moto mkubwa umeibuka Januari mwaka huu.

Moto wa asili si jambo geni kwa Tanzania na itakumbukwa kwamba mwaka 2023 ulilipuka katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na kuvuruga uoto wa asili na shughuli za kitalii pia.

Japo mara nyingi moto unahusishwa na moto wa asili.

## WATAFITI WANAKUPAKULIA MAPYA, UKIVUTA 3 UMEKATA SAA 1 YA UMRI WAKO

**INATOKA UK.11**

za matunda ili kuwapumbaza watumiaji hasa vijana ili wafurahie kutumia bila kupima madhara makubwa ya kiafya.

Mara kadhaa, wanaharakati na madaktari bingwa nchini wameonya kwamba kwa hali ya matumizi ya shisha, sigara za kielektroniki na aina nyingine za tumbaku, miaka michache ijayo Tanzania itakuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa moyo na saratani wenye umri mdogo.

Bingwa wa magonjwa ya mfumo wa upumuaji kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Mwanaada Kilima, mara kadhaa anasema asilimia 90 ya saratani ya mapafu na koo inatokana na matumizi ya tumbaku wakati bidhaa hizo zikichangia asilimia 40 ya aina nyingine ya saratani.

"Nimeona madhara mengi na makubwa sana...matumizi ya tumbaku ya aina yoyote ile iwe ya kusokota, kumung'unya, sigara au za kielektroniki ni majanga," anasema.

Mbali ya saratani, madaktari wanaeleza kuwa mtu anapovuta sigara, ndani ya saa moja presha yake na mapigo ya moyo yanapanda kwa kasi na athari ya hali hiyo ni shinikizo la juu la damu, mishipa ya fahamu, ubongo na hata kupata kiharusi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Chama cha Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku Tanzania (TTCF), Lutgard Kagaruki, anasema athari za matumizi ya tumbaku zinajulikana kutokana na kusababisha maradhi ya saratani, moyo, kisukari na magonjwa sugu ya mfumo wa hewa huku watumiaji wakifariki mapema kabla ya umri wao.

"Tunajua tumbaku inaua kuanzia ya msokoto ya shambani, kufunga kwenye karatasi, ya kiwandani, sigara kielektroniki na shisha. Zote hizi ni tumbaku na zinapunguza umri wa kuishi na kusababisha mzigo kwa familia na jamii kutokana na maradhi yanayowapata watumiaji," anasema Kagaruki.

Anasema viungo vinavyowekwa kwenye tumbaku vimesababisha madhara ya muda mfupi na mrefu, ikiwamo kifua kubana na mwisho kupata saratani ya mapafu na mishipa ya damu kuvimba.

Anaonya kwamba wakati matumizi ya tumbaku yakipungua katika baadhi ya nchi, hali ni tofauti nchini kwani yanaongezeka yakiwaathiri zaidi vijana kutokana na watengenezaji kuongeza vionjo vya ladha hasa kwenye shisha.

"Kama hakuna hatua madhubuti zitakazochukuliwa, miaka mitano au 10 ijayo, kwa kiwango ambacho vijana wanavuta shisha na sigara za kielektroniki, Ocean Road, Muhimbili na hospitali nyingine kwenye kliniki za kisukari hakutatosha. Tuna vijana ambao wanaelekea kupata uraibu kutokana na matumizi holela ya shisha," anasema.

Anaongeza: "Ukikaa karibu na wanaovuta shisha ndani ya saa moja hata kama hutumii, ni sawa na umevuta vipisi 100 vya sigara. Anayetumia shisha ni sawa na amevuta sigara 200."

Anasema imethibitika kwamba tumbaku inasababisha magonjwa mengi yanayozuilika ikiwamo afya ya akili na uraibu wa dawa za kulevya.

"Kuna ongezeko la vifo vya vijana kutokana na magonjwa ya figo, mapafu, shinikizo la damu, saratani, kisukari, magonjwa ya fahamu na afya ya akili. Kama nchi tunaelekea sehemu mbaya sana kwa sababu nguvu kazi ya taifa inapotea. Vijana wanavuta sigara na wanatumia pombe kali," anasema Kagaruki.


Anaishauri serikali itunge sheria kali kudhibiti matumizi ya tumbaku na kupiga marufuku kuvutaa shisha.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Kupata kiu ya sekondari nyingi za sayansi, kwa wagusa wananchi

• Wanakijiji waanza ujenzi kwa kasi




Mbunge wa Musoma Vijijini (kulia), Profesa Sospeter Muhongo akiwa na walimu pamoja wanafunzi baada ya kuwagawia vitabu katika Shule ya Sekondari Mugango. **PICHA: MTANDAO**

WILAYA ya Musoma ni moja ya wilaya za mkoa wa Mara, hasa jimbo la Musoma Vijijini, wana habari njema katika mikakati ya elimu 2025, ambayo ni kuinua masomo ya sayansi kwa kila kata.

Wananchi wamedhamiria kutenga sekondari mbili za kata za kidato cha tano na sita kwa ajili ya mchepuo wa masomo ya fizikia, kemia, hisabati, bailojia na jografia.

Ndivyo anavyosema Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Majidu Karugendo.

Anazitaja kuwa ni Sekondari ya Suguti itakayokuwa na mchepuo wa fizikia, kemia na hisabati (PCM), fizikia, kemia na bailojia (PCB), kemia, bailojia na jiografia (CBG) na uchumi, jiografia na hisabati (EGM).

Nyingine ni Sekondari ya Mugango ikitarajiwa kuwa na mchepuo wa kemia, bailojia na jografia (CBG) na EGM.

Ofisa elimu anasema hayo wiki iliyopita, wakati akizungumzia mikakati ya kuinua masomo ya sayansi kwenye sekondari za halmashauri yake, ili kuandaa wataalam wengi zaidi wa baadaye wa fani mbalimbali watakaolifikisha taifa kwenye dunia ya sayansi na teknolojia.

"Lengo letu ni kutaka kuinua masomo ya sayansi kwa wanafunzi wa Musoma Vijijini na halmashauri yetu ili kuandaa wataalamu wa fani mbalimbali wa baadaye," anasema Karugendo.

Anafafanua kuwa sekondari hizo kila moja ina maabara tatu za masomo ya sayansi, bweni moja au mawili, maji na umeme, na kwamba hatua hiyo itasaidia wanafunzi kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo.

"Mwaka huu sekondari hizo zitakuwa na 'high school' kwa masomo ya sayansi, hivyo tunatamani kuona hilo linatimia ili kuwa na vijana wengi wabunifu kupitia masomo hayo kutoka huku kwetu," anasema.

Aidha, anasema wakati kukiwa na mkakati huo wa kuzifanya baadhi ya sekondari za kata kuwa za kidato cha tano na sita, huenda pia baadhi ya sekondari za vijiji zinazoendelea kujengwa zikafunguliwa mwaka huu.

"Mfano kuna sekondari za Muhoji, Rukuba Island, Nyasaungu, Butata, Nyamrandirira Technical na David Massamba Memorial, zitakazokidhi vigezo ikiwamo kuwa madarasa ya kutosha kuchukua wanafunzi, zitafunguliwa kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza," anasema.

Anafafanua kuwa kila sekondari imepokea Sh. milioni 584, kutoka serikalini za kuanza ujenzi, na kwamba kuna vijiji vingine sita ambavyo navyo vimepata vibali vya kujenga sekondari.

Ofisa elimu huyo anavitaja vijiji hivyo kuwa ni Chitare, Katakkryo, Kiriba, Mmahare, Musanja na Nyambono, huku akiongeza kuwa itafika wakati kila kijiji kitakuwa na sekondari yake.

Musoma Vijijini ipo ndani ya halmashauri yetu ina vijiji 68, kata 21 na sekondari 24 za serikali na mbili za binafsi, kwa mwamko wananchi wa kuinua elimu, ninaami kila kijiji kitakuwa na sekondari yake," anasema.

### JICHO LA MBUNGE

Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, anasema vijana wa Kitanzania wakiwamo wa jimboni mwake, wanapaswa kujiandaa kuingia katika ushindani wa dunia ya sasa na ijayo wa ajira, taaluma, ubunifu na uchumi.

"Maoteo au global forecast, ifikapo mwaka 2030, utakuwapo upungufu wa wataalamu milioni 80 ifikapo mwishoni mwa mwaka huo, kampuni kubwa duniani zitatumia takribani Dola za Kimarekani trilioni 3.2, kila mwaka kuwekeza kwenye akili bandia au akili mnemba (Artificial Inteligence -AI)," anasema Prof. Muhongo.

Anaeleza kuwa, kampuni zitafanya hivyo, ili kutatua tatizo la ukosefu wa wafanyakazi duniani, na kwamba roboti zitatumika kwa wingi, na kwamba ni muhimu kuwekeza katika masomo ya sayansi.

"Tunaanza na sekondari chache, lakini zinahitajika nyingi zaidi. Kwa mfano sekondari za Bugwema, Nyakatende, Kiriba na Etaro ambayo ina chumba cha kompyuta, zote zina maabara tatu," anasema.

Mbali na hizo, mbunge huyo anazitaja nyingine zinazolengwa kuwa na kidato cha tano na sita kuwa ni Rusoli, Makojo na Nyambono, ambazo anasema kila moja ina maabara mbili.

"Wanavijiji wanaowamba wadau elimu wakiwamo wazaliwa wa Musoma Vijijini waishio maeneo mbalimbali, waendelee ushirikiana na serikali kuchangia ujenzi wa maabara za masomo ya sayansi katika sekondari za jimboni humu ili kuboresha masomo ya sayansi.

### MFUKO WA JIMBO

Mbunge huyo anasema fedha za mfuko wa jimbo ni Sh. milioni 75.7 na kwamba zimetumika kwa ajili ya vifaa vya ujenzi katika sekondari mbalimbali za kata na vijiji jimboni humo.

"Wiki iliyopita, Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilitembelea ofisi za halmashauri yetu zilizopo Kijiji cha Suguti kwa ajili ya kuweka mikakati ya kununua vifaa vya ujenzi kwa ajili ya shule mbalimbali," anasema.

Prof. Muhongo anavitaja baadhi ya vifaa hivyo kuwa ni mifuko 1,970 ya saruji, mabati ya rangi 322 na nondo 430 za milimita nane, huku baadhi ya shule zitakazofaidika zikiwa ni Muhoji na Nyasaungu.

Mbali na hizo, nyingine ni Rukuba na zile zinazokamilisha ujenzi wa maabara za masomo ya sayansi zikiwamo za Mtiro, Makojo, Nyambono, Bwai, Mkirira, Etaro na zinazoanza ujenzi wa maabara za masomo hayo za Bukwaya na Nyanja.

"Katika mgawo huo zimo pia sekondari za Chitare, Mwigombe, Mmahare, Musanja, Kataryo, na Nyabakangara ambazo wananchi wa maeneo hayo wapo kwenye harakati wa ujenzi," anasema.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Zingatia haya kuandaa watoto kukurithi iwapo utatwaliwa

- Lengo kulinda kazi, kuendeleza mali na utajiri uliouanzisha

MWAKA 2025 huu hapa. Wewe ni mmiliki wa migodi, viwanda, ardhi, mazao na mifugo. Ikitokea umetwaliwa je, umeandaa watoto wako kurithi na kuendeleza mali zako?

Kama hujafanya hivyo fikiria uanze sasa ikiwezekana. Ni kwa sababu kuna madai kuwa kama wazazi na walezi wenye mali au utajiri wakifa, wameondoka na mali zao.

La msingi usiwabague watoto kijinsia wanawake na wavulana wape nafasi sawa.

Hakuna wakuziendeleza mara nyingi zitauzwa ili kugawana mali, zitafilisika na kusahaulika na migogoro mingi ya kugombania fedha, itafikishwa mahakamani kesi nyingi zikifunguliwa na kuwapo malalamiko hata ya wanafamilia kujiua.

Sababu mojawapo ni wazazi na walezi kushindwa kuwapa watoto mbinu au mikakati ili kuwaandaa kurithi na kuendeleza majukumu yao, pale watakapofariki au kuumwa na kushindwa kuendeleza juhudi walizoanzisha.

Ni dhahiri yapo malezi kwa watoto kuwaandaa na hatima kubwa ya kuendeleza biashara au hata mali na kuiongoza familia kwenye uwekezaji.

Watanzania au 'Wabongo' wanafahamu na wanaona baadhi ya jamii mfano Wazungu, Waarabu na watu wengi wenye asili ya Asia kama China, India wanavyowaandaa watoto wao kuwa warithi wa biashara na miradi ya uwekezaji.

Ni juhudi zinazofanywa mapema katika ukuaji wao. Unaweza kuwakuta watoto wakiuza madukani, au kuwa kwenye maeneo ya uzalishaji katika utoto wao ili kuelewa aina ya biashara.

Katika eneo hilo zipo pia familia zinazowaandaa watoto pengine kwa kuchagua mmoja maalum ambaye hutayarishwa kuwa kiongozi wa biashara, uwekezaji na familia nzima.

Pengine kwa Afrika hakuna juhudi kubwa zinazoonekana hivyo Watanzania wana haja ya kufanya jambo hilo ili kuendeleza na kudumisha mambo bora ya kiuwekezaji na haki za kumiliki na kutunza utajiri wa familia hata baada ya wazazi na walezi kuondoka.

Ethiopia na Somalia kuna jamii zinazofanya jambo hilo, lakini kwa Watanzania utamaduni huo haujafanikiwa na kuacha alama za watu kujifunza, japo kuna baadhi wameweza kuwaachia watoto wao biashara na urithi wa mali.




Kama ni mkandarasi wa barabara watoto wako wawe sehemu ya wahandisi wajenzi. **PICHA: MTANDAO**

Nipashe imefuatilia kesi za mirathi mahakamani na kuona kuwa kitu kinachoshitua ni pale walezi wanapokosea katika kupenyeza maarifa, ujuzi wa biashara na usimamizi wa mali hizi kwa watoto ili kuwaandaa kuwa warithi wa sasa na miaka ijayo.

Tujiulize ni nini jamii nyingine zinafanya ambazo sisi Watanzania hatufanyi? Kwanini leo kuna biashara kubwa ambazo zinaishi karne nyingi mpaka zimesambaa dunia nzima kutoka kwa mwanzilishi, watoto na sasa ni kwa wajukuu hata vitukuu?

**YAKUZINGATIA**

Kuandaa kizazi chako chenye ushindi kuna vitu unatakiwa uvizingatie tangu wanapoanza kukua na kitaalamu jukumu linaloitwa 'grooming' ambalo linahusisha kile mtoto anachobeba tangu utotoni.

Watu wakumbuke kuwa hata kama utaacha wosia kama hujatengeneza kizazi cha ushindi mali na biashara zipo hatarini. Haziwezi kufika mbali pengine zitakwamia kizazi cha pili.

**KUTAWALA PESA**

Mtoto anaandaliwa kuitawala na kuiheshimu pesa na siyo pesa imtawale au kumzuzua. Katika mambo ambayo jamii ya leo yanamaliza vijana wengi ni kushindwa kuitawala pesa, ni somo ambalo halifundishwi shuleni au chuo chochote.

Inashangaza hata wanaosoma masomo ya biashara wanashindwa kuiweka chini ya miguu yao, hivyo wafundisheni watoto wakiwa na pesa wanapaswa kuzipeleka sehemu gani.

Anatakiwa kununua vitu gani vya faida gani kwake, maamuzi yake anapokuwa na pesa mkononi ni yepi? Anafanya nini na kwa wakati gani?

Katika kumwandaa mtoto mpe pesa na umuone anakimbilia kununua nini, mara nyingi wazazi na walezi wanawapa pesa watoto na wanakimbilia kununua pipi, biskuti, soda na wanataka baiskeli.

Umeshawahi kujiuliza mtoto ukimwelezea kinyume na hayo anaweza kuweka akiba yake mwenyewe, hata kama anahitaji baiskeli? Tengeneza naye bajeti mwambie tunaanza kuweka akiba ya baiskeli ashiriki na aone kuwa yeye anaweza kuitawala pesa.

Kama utashindwa kumfundisha kutawala pesa atafanya ufujaji ataona mali ni nyingi siku atakayoipokea mikononi mwake, atakimbilia kuimaliza na kuishia kufilisika.

**VIKAO KUHAKIKI**

Suala jingine la kumwandaa mrithi ni kuwa na vikao vya mara kwa mara ukiwa na mtoto kwenye usimamizi wa biashara, mali, kama mashamba, mifugo, ardhi, maduka, hospitali na viwanda au kampuni za huduma.

Mali hailindwi na mikono milegevu, kadhalika biashara hailindwi wala kutunzwa na mikono legevu, nguvu unayotumia kuwekeza katika mali zako na utafutaji wako hakikisha nguvu hiyo mtoto anaiona na unamwambukiza.

Kama ni shamba unakwenda kukagua mifugo au mazao hakikisha unakwenda naye mara kwa mara aone nini unachofanya, makubaliano unayoingia na wafanyakazi au washirika mbalimbali.

Lakini mzazi au mlezi unapomwandaa mtoto hakikisha unamwambia aangalie unachofanya na baada ya hapo ingia naye kwenye maongezi ya nini alichojifunza.

Kama ni biashara unafanya hakikisha unakwenda pamoja naye mwishoni mwa wiki na anashiriki, kama mtoto anaweza kuangalia video au katuni na akavutiwa eelewe unachomjengea pia atakishika, unatengeneza kiongozi anayejua anachofanya hata kama atapata changamoto, atakumbuka.

Mfundishe mtoto uaminifu, uthubutu, ujasiri, maadili na walezi na wazazi wengi wanawarudisha nyuma watoto kwa kuwanyima kufanya mambo ambayo wanahisi umri wao bado au wanaona ni kupoteza muda.

Hakuna sababu ya kuwakatisha tamaa watoto wanapoonyesha ubunifu na uthubutu wa aina yoyote wapewe nafasi na uungwaji mkono na kusifiwa kuwa anaweza.

Ikiwezekana shiriki naye katika anachofanya, biashara haitaki kichwa kilicholala inataka moyo wenye uthubutu na akili ambazo utaweza kukupeleka mbele.

Uthubutu ni taarifa kuwa yupo imara kwa utayari kwa mapambano mfundishe kufanya kazi kwa bidii na umfundishe kukataa uvivu, kama mzazi hukutenda kazi kwa mikono milegevu na umepitia mapito mengi mpaka kupata mali na mafanikio ni dhahiri kwamba maisha ya binadamu umefahamu kuwa sio lelemama.

Mikono milegevu huipoteza mali, watoto wafundishwe kufanya kazi na sio tu kazi ni kufanya kwa bidii na kukataa uvivu kabisa katika maisha yao.

Maisha ya vijana wengi tunayaona wanavyotaka vitu rahisi na kugubikwa na uvivu, hivyo lazima watoto wafunzwe kuweka akilini kuwa uvivu ni tatizo na ndicho kinachoangusha maisha ya wengi.

Hilo linafanikiwa kwa kushiriki naye kazi za nyumbani, kumpangia majukumu na kumwamsha mapema kwa mazoezi katika utoto wake.

**NIDHAMU LAZIMA**

Wazazi na walezi wafundisheni nidhamu watoto au warithi na kuachilia mbali nidhamu ya pesa fundishe mwanao nidhamu ya kujiheshimu, kumheshimu kila mmoja anayemzunguka na kujali muda, katika biashara nidhamu imebeba asilimia zaidi ya hamsini ya mafanikio.

Yeyote anayeshindwa kuwa na nidhamu mafanikio yanakuwa magumu kwake, ni nguzo ya muhimu itakayomfanya ajue namna ya kuwasiliana na jamii katika ngazi mbalimbali.

Mfundishe uvumilivu na ustahimilivu, kama wewe mzazi wakati wa kutafuta mafanikio, fedha na mali ulipitia magumu, basi vivyo hivyo uamini kuwa magumu katika maisha ni sehemu ya nyakati za wote za mafanikio ni hakika pia mwanao atapita nyakati hizi, iwe una pesa nyingi za kutosha au hauna mwandae mwano kisaikolojia azitambue nyakati hizi na aweze kuwa mvumilivu na kustahimili.

Aidha, awe na uwezo wa kufanya maamuzi ya busara katika nyakati kwani ndipo ubora wake utakapoonekana. Tengeneza mazingira ya kumfanya aweze kustahimili mambo madogo nyumbani, mpeleke kwa ndugu kijijini aone mazingira magumu na aishi usimweke ndani eti hutaki mwanao apate shida.

Wakati mwingine nafasi za Jeshi la Kujenga Taifa JKT zikitoka hakikisha mpambanie aende anachopita huko kinamjenga, anapaswa kuona pande zote za maisha.

**LA MUMIHU**

Kuandaa mtoto haijalishi uwe mfanyabiashara mkubwa au mdogo au mfanyakazi ni jukumu la kila mzazi au mlezi katika ngazi yoyote, mfano unaodhihirika wanaofanya hili pia na wanafanikiwa kuwapenyeza watoto wao ni wanasiasa.

Ukiwaangazia wanakupa taswira halisi nini wanafanya kwanini wewe ushindwe, tengeneza kizazi chako cha ushindi sasa, linda jasho na mali zako watoto hawatasahau njia na maarifa yako.



# Tume yapeleka neema kwa wakulima Kongwa

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

TUME ya Umwagiliaji Mkoa wa Dodoma imewahakikisha wakulima wanaotumia Skimu ya Umwagiliaji ya Tubugwe Juu wilayani Kongwa kuwa wataalamu wake wako bega kwa bega kuhakikisha Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP - P4R) unaleta tija kwao.

Kauli hiyo imetolewa na Mhandisi wa Tume hiyo wa mkoa huo, Osward Urassa kwenye Mkutano Mkuu wa wakulima hao na utiaji saini mkataba wa usimamizi, uendeshaji na matunzo ya skimu hiyo kwa lengo la kuwainua kiuchumi.

Alisema hatua hiyo ni ishara kuwa serikali imejipanga kuona wakulima wanaufaika na uwekezaji huo.

"Tume itaendelea kutoa ushirikiano kuanzia ngazi ya wilaya hadi mkoa, tunahitaji kuona wakulima wananufaika na uwepo wa Skimu ya Umwagiliaji ya Tubugwe Juu," alisema Urassa.

Alisema skimu hiyo yenye ukubwa wa ekari 375, inanufaisha wakulima 186 wa vijiji vya Mongwa, Tubugwe Kibaoni na Bumila wilayani humo.

Skimu hiyo ni miongoni mwa 23 nchini zinazonufaika na mradi huo wa TFSRP - P4R.

Mwenyekiti wa skimu hiyo, Zuberi Mwagillo, alisema kuwapo kwa mradi huo kutarejesha matumaini ya wakulima hao na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao maeneo ya vijiji vya wilayani humo.

**Mwagillo, alisema wataendelea kutoa ushirikiano kwa tume hiyo ili kufanikisha lengo la kukifanya kilimo cha mazao hayo kwa njia ya umwagiliaji kinakuwa endelevu kwa faida ya wakulima hao ...**

Mwagillo, alisema wataendelea kutoa ushirikiano kwa tume hiyo ili kufanikisha lengo la kukifanya kilimo cha mazao hayo kwa njia ya umwagiliaji kinakuwa endelevu kwa faida ya wakulima hao na vizazi vijavyo.

Mwenyekiti huyo aliishukuru NIRC kwa kuchagua skimu hiyo kuwa miongoni mwa zitakazonufaika na TFSRP - P4R nchini.

Mwagillo, alisema kwa kipindi kirefu wakulima hao walipoteza matumaini ya kuendesha kilimo chenye tija kutokana na kushindwa kufanyika ukarabati miundombinu baada ya kuharibiwa na maji, hivyo, utiaji saini matunzo na usimamizi wa skimu hiyo umeamsha ari ya kuongeza uzalishaji wa mazao maradufu.

Pamoja na mambo mengine, aliishukuru NIRC kwa kuwapa wakulima elimu ya utekelezaji mradi huo na kutatua changamoto katika skimu hiyo.

Aliwataka wakulima kuendesha kilimo chenye tija kwa kushirikiana na tume hiyo baada ya kuahidi kuwa mstari wa mbele kuwahakikishia utunzaji na usimamizi bora.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi, akizungumza na viongozi kabla ya kugawa hati miliki zilizotolewa juzi kwa wakazi wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Samia achangia ujenzi wa msikiti

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametekeleza ahadi yake ya kutoa Sh. milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa msikiti wa Taqwa mkoani hapa.

Fedha hizo zimetolewa kupitia Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Ally Hapi.

Katibu wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Singida, Omari Muna, alikabidhi hundi ya malipo ya fedha hizo jana kwa Sheikh wa Mkoa huo, Issa Nassoro katika hafla iliyohudhuriwa na Mkuu wa Mkoa, Halima Dendego na waumini.

Akizungumza kwa njia ya simu katika hafla hiyo iliyohudhuriwa na Mkuu wa Mkoa huo, Halima Dendego na waumini wengine, alisema Rais Samia amekuwa akisaidia ujenzi wa misikiti na makanisa kutokana na mapenzi makubwa aliyonayo kwa Watanzania.

Alisema wananchi nao wanatakiwa warudishe shukrani kwa Rais Samia kwa kuendelea kumwombea kwa Mungu awe na afya njema na kuongoza taifa kwa amani na utulivu.

Alisema fedha hizo zitumike vizuri kwa malengo yaliyokusudiwa ili rais na wadau wengine waone umuhimu wa kuendelea kuchangia zaidi ujenzi wa msikiti huo na nyumba zingine za ibada nchini.

"Niwaombe tuendelee kumwombea dua na afya njema rais wetu kwani mambo anayoyafanya ni kutokana na mapenzi makubwa aliyokuwa nayo kwa Watanzania, ninampongeza Sheikh wa Mkoa kwa kuwashirikisha waumini katika suala hili la ujenzi wa msikiti," alisema Happi.

Sheikh Nassoro, alimshukuru Rais Samia kwa mchango wake huo na kuwataka wananchi kuendelea kumuunga mkono kutokana maendeleo anayoyafanya nchini.

Aliwataka wananchi kuwapuuza watu wamekuwa na tabia ya kubeza mambo mazuri ya maendeleo aliyofanya rais kwa kipindi kifupi.

Aliwasihi wananchi katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2025 waendelea kudumisha amani na upendo ili kuwaenzi waasisi wa Taifa la Tanzania.

" Mwaka 2025 tunaenda kwenye uchaguzi, tutazame kuchagua viongozi waadilifu kama alivyo Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Sheik Nassoro.

Kwa upande wake Dendego, alimshukru Rais Samia kwa mchango huo wa ujenzi wa msikiti na kumuunga mkono kwa kutoa Sh. milioni 5.

"Tunawashukuru wale walioguswa kuchangia ujenzi wa msikiti huu, mpaka sasa zimefikia Sh.milioni 176 na kila mmoja apate baraka za Mungu," alisema.

Alisema malengo ya ujenzi huo bado hayajafikiwa na kuwaomba waumini wa dini hiyo na wadau wengine waendelee kuunga mkono kufanikisha.

Naye Muna, alisema atahakikisha miradi yote inayoetekelezwa inakwenda vizuri ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha Waislamu wa mkoa huo.

# Maandalizi utoaji chanjo yapamba moto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amezindua gari na pikipiki tisa kusambaza chanjo katika vituo vya afya vya halmashauri saba za mkoani hapa.

Akizungumza kwenye hafla ya uzinduzi huo, Senyamule aliagiza vyombo hivyo vya moto kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na si vinginevyo.

"Tuna mshukuru Rais wetu (Samia Suluhu Hassan kwa gari hili pamoja na pikipiki hizi ambazo zitasaidia kuondoa changamoto iliyokuwapo awali ya kukosa usafiri," alisema Senyamule.

Alisema kupatikana kwa vyombo hivyo vya moto, kutasaidia pia kutoa elimu kwa wananchi kuondokana na magonjwa ikiwamo ya mlipuko.

Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk.Thomas Rutanzibwa, alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka na kurahisisha usambazi wa chanjo katika maeneo ya mkoa na kuwafikiwa wananchi kwa wakati na kwa idadi kubwa.

# Wazazi wakumbushwa kupiga vita adui ujinga

**Na Elisante John,** SINGIDA

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kati, Usharika wa Amani mkoani hapa limewataka wazazi na walezi kusimamia maendeleo ya elimu kwa watoto wao waliojiunga na kidato cha kwanza na elimu ya awali na msingi ili kuunga mkono juhudi za serikali kupiga vita adui ujinga nchini.

Mwinjilisti wa Usharika huo, John Jambi alitoa rai hiyo wakati wa ibada iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita.

Jambi, alisema licha ya Wakristo kutakiwa kudumisha amani na upendo, wametakiwa kuunga mkono mafanikio ya elimu yanayotokana na mageuzi makubwa yanayofanywa na serikali. Alisema lazima wazazi, walezi na jamii kuhakikisha wanafunzi wenye sifa, waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu baada ya kufaulu mitihani ya darasa la saba mwaka jana, wanaripoti kwenye shule walizopangiwa, kuanza masomo wiki hii.

"Naomba tumuunge mkono Rais wetu anayependa elimu, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha tunawapeleka watoto wetu wote waliofaulu kidato cha kwanza, na wale wanaoanza elimu ya awali na msingi wakaanze masomo, " alihimiza Mwinjilisti huyo.

Alifafanua kuwa Rais Samia ameboresha miundombinu ya kujifunzia ikiwemo ujenzi wa shule mpya za sekondari na msingi, hivyo ni wajibu wa kila muumini wa KKKT na jamii kuunga mkono juhudi hizo kwa kupeleka watoto shule na kupiga vita adui huyo ujinga.

KKKT Amani umekuwa ukipokea wanafunzi wapya katika shule yake ya Hosanna.



# Waondolewa adha kubeba wagonjwa kwa machela

**Na Mwandishi Wetu,**
BUSOKELO

SERIKALI imekabidhi gari la kubebea wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Mwakaleli cha Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya na kuachana adha ya kubebwa kwa machela.

Wakizungumza wakati wa kukabidhiwa gari hilo, wakazi wa eneo hilo, walisema litawasaidia kupunguza vifo kwa kuwahishwa kufika hospitalini kupata matibabu.

Mmoja wa wakazi hao, Retina Simbega, alisema kabla ya serikali kuwakabidhi gari hilo walikuwa wanalazimika kusafirishwa kwa kubebwa kwenye machela, pikipiki na kutembea kwa mguu kwenda hospitalini kupata matibabu.

Alisema tatizo kubwa lilikuwa kwa wajawazito ambao walikuwa wanapatiwa rufani ya kwenda Hospitali ya Wilaya na ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

**Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. Imamu Ugawa, alisema kabla ya kukabidhiwa gari hilo, wamepokea vifaa tiba mbalimbali kutoka serikalini.**

Alisema baadhi yao walikuwa wanajifungulia njiani na kusababisha vifo vya mama na mtoto kwa kukosa huduma haraka.

Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. Imamu Ugawa, alisema kabla ya kukabidhiwa gari hilo, wamepokea vifaa tiba mbalimbali kutoka serikalini.

Dk. Ugawa, alisema kituo hicho kinahudumia wakazi wa kata zote za Bonde la Mwakaleli.

Alisema hali ya mazingira ya eneo hilo, yanatakiwa kuwa na vyombo vya usafiri vya uhakika kwa ajili ya kuwahisha wagonjwa hospitali kupata huduma haraka ya matibabu.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Jaffar Haniu, alisema wamepokea magari matatu ya kubeba wagonjwa, likiwamo moja la kituo hicho.

Alisema kituo hicho cha Mwakaleli ni miongoni mwa vituo muhimu kulingana na idadi kubwa ya watu wanaoishi bonde hilo kuhitaji huduma za matibabu.



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Mlima Nji kilichoko Kata ya Mbugani wilayani Chunya, Mkoa wa Mbeya, wakiangalia mizoga ya ng'ombe ya mmoja wa wafugaji wa kijiji hicho wanaodaiwa kufa baada ya kunywa maji yenye kemikali za sumu zilizotiririshwa kutoka kwenye moja ya mitambo ya kuchenjulia dhahabu mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wananchi wajengewa mradi wa maji safi

**Na Nebart Msokwa,**
KYELA

WAKAZI wa kata 15 za Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wameondokana na adha ya kutumia maji ya kisimani na mtoni baada ya serikali kukamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wenye thamani ya Sh. bilioni 4.1.

Wakazi hao wanadai kuwa kabla ya ujenzi wa mradi huo kukamilika, walikuwa wanatumia maji hayo na kusababishia baadhi yao kuugua magonjwa ya tumbo na kipindupindu.

Mradi huo unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela, unatarajiwa kunufaisha wakazi hao wa kata zote za Kyela Mjini na baadhi ya maeneo ya pembezoni.

Wakizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo uliofanyika Kata ya Itope, waliishukuru serikali kwa kuwanusuru kukumbwa na magonjwa hayo na kipindupindu na kuwaondolea adha ya kuhangaika kutafuta maji kwa muda mrefu.

Sela Mwakaje, alisema katika eneo hilo kulikuwa na tatizo kubwa uhaba wa maji hasa wakati wa kiangazi.

Sela, alisema hata visima walikokuwa wanahemea maji, vilikuwa vinakauka, hivyo kuwalazimu kwenda kutafuta kwenye mito.

Alisema kutokana na hali hiyo, hali yao ya maisha ilikuwa ngumu kwa kulazimika kusitisha shughuli za uzalishaji mali na kwenda kusaka maji. "Wakati kama huu tunakinga maji ya mvua na tunayatumia kunywa, lakini kiangazi hali huwa ni ngumu sana kwa sababu visima vyetu vinakauka kabisa," alisema Sela. Alisema kero hiyo ilikuwa inawatesa zaidi wanawake na watoto kwa kuhangaika kwenye mito kuchota maji na kuhatarisha maisha yao.

Fred Sanga, alisema maji waliyokuwa wakiteka kwenye visima si salama kwa afya zao kwa kuwa yalisababisha baadhi ya kukumbwa na magonjwa hao kutokana na kuwa jirani na vyoo.

Aliishukuru serikali kwa kujenga mradi huo na kutatua kero ya ukosefu wa maji ambayo ilikuwa inawasumbua kwa muda mrefu kwenye maeneo yao.

"Tunaomba serikali iendelee kukamilisha mradi huu katika maeneo yaliyoabakia ili wananchi wengi zaidi wanufaike," alisema.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Raphael Francis, alisema ukikamilika kwa asilimia 100, utahudumia zaidi ya wakazi 127,000 wa kata hizo.

Francis, alisema mahitaji ya maji kwa wakazi hao ni zaidi ya lita milioni tisa kwa siku. Alisema sasa uzalishaji wa maji ni lita milioni tano sawa na asilimia 60 ya mahitaji ya wakazi hao.

Akizindua mradi huo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Josephine Manase aliitaka Mamlaka hiyo kuusimamia vizuri ili uwahudumie wakazi hao kwa muda mrefu.

Josephine, vilevile aliwataka wakazi hao kulinda miundombinu ya mradi huo na kuhakikisha wanalipa ankara kwa wakati ili uendelee kuhudumia jamii.

# Mamlaka yatakiwa kutolea elimu kwa wadau

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) imetakiwa kuendelea kutoa elimu kwa wadau wa nafaka na mazao mchanganyiko kuinua kipato cha wakulima na wafanyabiashara nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Salum Hamdun wakati akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa COPRA, Irene Mlola ofisini kwake baada ya kwenda kuitambulisha mamlaka hiyo mkoani humo.

Hamduni, alisema COPRA ikiendelea kutoa elimu kwa wadau, itasaidia zaidi kwa wakulima na wafanyabiashara kutumia mifumo hiyo kutatua changamoto zao kwenye ununuzi na uuzaji wa mazao hayo.

"Hongereni kwa kazi mnayofanya, lakini endeleeni na utaratibu wa kukutana na wadau ili utekelezaji wa majukumu yenu uende sambamba na uelewa wa wadau wote katika mnyororo wa thamani wa nafaka na mazao mchanganyiko," alisema na kusisitiza kuwa:

"COPRA ni ya muhimu sana ndani ya jamii inayotuzunguka, jitihada zaidi zinahitajika kuelimisha jamii kuhusu mamlaka hiyo ili waweze kuitumia kutambua changamoto kwenye mazao mchanganyiko."

Hamduni, alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya kilimo na kuwataka wakulima na wafanyabiashara kutumia mamlaka hiyo kutatua kero zao na jamii katika upatikanaji wa chakula kwa bei nafuu.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa COPRA, Irene alimweleza Mkuu huyo wa mkoa kuwa mamlaka hiyo itaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa kwenye mnyororo wa thamani wa nafaka na mazao mchanganyiko.

Alisema maofisa wa COPRA watafanya kazi kwa kushirikiana na viongozi na wataalamu wengine wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha wakulima na wafanyabiashara wanaitambua mamlaka hiyo.

Alilitaja lengo lingine kuwa ni COPRA kushirikiana na wakulima na wafanyabiashara hao ili waweze kutambua mnyororo wa thamani wa mazao hayo nchini.

Mamlaka iliyopo Wizara ya Kilimo, imejipanga katika urasimishaji wa biashara hiyo nafaka na mazao mchanganyiko kupitia mifumo iliyowekwa na serikali.

Lengo la serikali kuanzisha mamlaka hiyo ni kuwainua wakulima na wafanyabiashara hao kiuchumi na kukabiliana na walanguzi wa mazao kwa kutumia vipimo batili vikiwamo lumbesa na kangoda.

# UWT yahamasisha wanawake kujiandikisha kupiga kura

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

UMOJA wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) umewataka wanawake kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika awamu ya mwisho ya daftari la kudumu la wapigakura mwezi ujao ili washiriki katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika nchini mwaka huu.

Rai hiyo imetolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja huo Zanzibar, Tunu Juma Kondo, wakati akizungumza na wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Tunu, alisema daftari hilo ni kigezo muhimu cha kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchaguzi huo rais, wabunge, wawakilishi na madiwani wa CCM na wa vyama vya upinzani nchini.

Alisema bila ya kujiandikisha katika daftari hilo ni vigumu kwa mwananchi yoyote kushiriki katika uchaguzi huo wa viongozi hao wa wakuu wa taifa, majimbo, kata na shehia. "Kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ndiyo mfumo pekee ambao utawawezesha wananchi kushiriki katika uchaguzi mkuu wa kidemokrasia kuchagua viongozi kwa mujibu wa sheria," alisema Tunu.

> **"Kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ndiyo mfumo pekee ambao utawawezesha wananchi kushiriki katika uchaguzi mkuu wa kidemokrasia kuchagua viongozi ...**

Baadhi ya wajumbe wa baraza la wawakilishi Zanzibar wa CCM waliahidi kufanya kampeni nyumba kwa nyumba kuhakikisha wananchi wenye sifa wanajiandikisha katika daftari hilo hivi karibuni. Mwakilishi wa Viti Maalumu wa Wazazi, Saada Ramadhan Mwendwa, alisema kazi ya kushawishi wananchi kujiandikisha katika daftari hilo imeanza ngazi zote katika Wilaya ya Magharibi.

"Wito wangu wanawake na vijana ambao hawajaandikishwa katika daftari la kudumu awamu iliopita wajitokeze awamu hii ili waweze kupiga kura kwa mujibu wa sheria," alisema.

Mwakilishi wa Viti Maalumu Wanawake mjini Magharibi Unguja, Sabiha Filfil Thani, alisema wanawake wengi katika Jimbo la Kikwajuni na shehia zake, walijitokeza kujiandikisha katika daftari hilo awamu ya kwanza mwaka jana.

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) inatarajia kuanza tena kuandikisha wananchi katika daftari hilo Februari mwaka huu katika hatua ya mwisho kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.



Mkuu wa Wilaya ya Rorya mkoani Mara, Dk. Halfan Haule (kulia), akikagua maendeleo ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Owak iliyopo Kijiji cha Kowak juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wizara, washirika kuwasaidia wakulima

Na Mwandishi Wetu,
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesisitiza itaendelea kuunga mkono jitihada za washirika wa maendeleo na kuwasaidia wakulima ili wapate tija katika kazi zao.

Mratibu wa Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania kwa upande wa Zanzibar, Sihaba Haji Vuai aliyasema hayo aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya mabibi na mabwana shamba, maofisa ugani wa wilaya na maofisa ushirika wa wilaya za Unguja mjini hapa.

Vuai, alisema mafunzo hayo yanalenga kuboresha kilimo nchini na wakulima kupata masoko ya uhakika.

Alisema mafunzo hayo yatawajengea uwezo katika usimamizi kwa wanawake na vijana waliojiunga na vyama vya ushirika vya kuzalisha na kuuza mazao ya mboga na kuinua kipato chao.

Vuai, aliwataka washiriki hao kutumia mafunzo hayo kuelekeza na kuwezesha makundi hayo kutafuta na kupata masoko kwa wakati na kwa urahisi.

Ofisa Kiungo Elimu kwa Wakulima wa Mradi huo, Saada Seif Said, alisema wakulima wa Zanzibar wanaendesha kilimo cha mbogamboga kwa mazoea, hivyo kutolewa kwa elimu hiyo kwa washiriki hao kutawasaidia kuachana nacho kwa kuanza kufuata taratibu za kilimo.

Ofisa wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika, Abdulmajid Masoud Khalfan, akizungumza kwa niaba ya washiriki wenziwe, alisema mafunzo hayo yatawawezesha kutambua namna ya kuzalisha bidhaa pamoja na utafutaji wa masoko.

# Tume yaanza kuchunguza vifo vya watu Pemba

Na Mwandishi Wetu

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Zanzibar imesema inachunguza vifo vya watu wawili vilivyotokea Mkoa wa Kaskazini Pemba mwishoni mwa mwaka jana ili kubaini chanzo chake.

Akitoa tamko la tume hiyo kwa waandishi wa habari ofisini kwake, Kamishna wake, Khatib Mwinchande, alisema imepokea kwa masikitiko makubwa vifo vya watu hao, Athuman Hamad Athuman (75) na Amour Khamis Salim (28), waliokuwa wakazi wa Kijiji cha Kiungoni, Wete kisiwani humo vilivyotokea Desemba mwaka jana.

Kwa mujibu wa Mwinchande, tume hiyo inalaani mauaji hayo kwa kuwa ni ukiukwaji wa haki ya mtu kuishi kama ilivyotamkwa katika Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Zanzibar.

Alifafanua kuwa ibara hiyo inaeleza kila mtu ana haki ya kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kwenye jamii kwa mujibu wa sheria.

Tamko la tume hiyo, linafuatia taarifa ya Jeshi la Polisi Mkoa huo ya Desemba 25 mwaka jana kuwa linaendelea uchunguzi wa vifo vya watu hao vilivyotokea wakati wakipatiwa matibabu Hospitali ya Ali Khamis Camp, Vitongoji Pemba.

Mwinchande aliendelea kusema kuwa mauaji hayo ya Kiungoni yametokea wakati tume yao inaendelea kufuatilia mauaji ya mengine yaliyokea Kaskazini Unguja na Tanzania Bara.

Alisema matukio hayo, yanarudisha nyuma juhudi za serikali kuimarisha ulinzi, amani na usalama wa raia na mali zao nchini.

Mwinchande, alisema kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, wakazi hao wa Kiungoni walikamatwa na askari wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya wakiwa hai kwa tuhuma za wizi wa baskeli na matumizi ya bangi na kurejeshwa siku ya pili wakiwa wamekufa.

Akizungumzia kuhusu utawala bora, Kamishna huyo, alisema mauaji hayo ni ukiukwaji wa msingi wa utawala bora hususan wa sheria.

Alisema dhamira ya tume hiyo ni kufanya uchunguzi wa tukio hilo na kuendelea na wa mengine kama hayo, kulinda misingi ya utawala bora na utawala wa sheria nchini.

"THBUB inawakumbusha wananchi na taasisi zote kupiga vita vitendo vyote vinavyokiuka sheria, misingi ya utawala na haki za binadamu, kwa kuwa haki ya kuishi ni haki ya msingi kwa kila mtu," alisema.



Katibu wa Baraza la Machifu Dodoma, Ndahani Chinang'anang'ana, akizungumza na machifu, makundi ya vyama vya siasa na viongozi mbalimbali wa dini alipokuwa akisisitiza umuhimu wa amani kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu kwenye mdahalo ulioandaliwa na Taasisi ya Wafikiriaji Duniani uliofanyika Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# CCT yahofu utitiri vibali kwa wafanyabiashara

**Na Maulid Mmbaga**

JUMUIYA ya Kikristo Tanzania (CCT) imesisitiza umuhimu wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kuonyesha urahisi wa sheria za biashara kwa kupunguza utitiri wa vibali ili kurahisisha uendeshaji shughuli hizo kwa wafanyabiashara na kuchochea maendeleo ya kitaifa.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa kamati ya dini mbalimbali, Mkurugenzi wa Programu za Maendeleo na Utetezi wa CCT, Azgard Stephen, alisema wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika kuhusu mlolongo wa vibali vinavyoambatana na masuala ya kodi, kuwa jambo hilo linasababisha wengi kukwepwa kulipa na kuathiri uchumi.

Pia, alishauri serikali kuliangalia suala hilo kwa kuweka utaratibu mzuri utakaowawezesha wafanyabiashara na Watanzania kulipa kodi kwa urahisi na haki, bila kushurutishwa.

"Sisi CCT tuliangalia suala la sayansi na teknolojia kwa kuzingatia jinsi dunia ilivyobadilika na mapinduzi yanayotokea. Tunapendekeza diplomasia iwe sehemu ya vichocheo vya maendeleo ili kuwezesha Tanzania kujihusisha vyema katika biashara za kimataifa na kujitengenezea nafasi bora kikanda na kimataifa," alisema Azgard.

Aidha, ni vizuri serikali iweka mkazo katika sekta binafsi kwa kuweka msisitizo wa kuwezesha mazingira mazuri ya uendeshaji biashara binafsi, badala ya kuangalia mashirika ya kijamii pekee.

"Pia mikakati ya utawala bora na kupunguza rushwa inapaswa kuangaliwa, lakini dira haijaiangalia rushwa kama kikwazo cha maendeleo, hivyo dira ionyeshe moja kwa moja kuwa rushwa ni adui wa maendeleo tuipinge," alisema.

> **"Pia mikakati ya utawala bora na kupunguza rushwa inapaswa kuangaliwa, lakini dira haijaiangalia rushwa kama kikwazo cha maendeleo, hivyo dira ionyeshe moja kwa moja kuwa rushwa ni adui wa maendeleo tuipinge," alisema.**

Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Sheikh Mohamed Khamis, alishauri kuwa ni vyema pia serikali iangalie namna ya kujiunga na mashirika ya kimataifa yanayoweza kusaidia katika kuchochea maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Alishauri kuingiza elimu ya rushwa katika mitaala ili watoto wawe na uelewa na kuipinga, kuboresha huduma za afya kwa kujenga vituo kuanzia ngazi ya mitaa hadi kijiji na kupunguza gharama za matibabu, na kuimarishwa kwa vitendo masuala ya amani.

"Kuboresha sekta ya utafiti pia ni muhimu ili kuibua fursa mpya, kusimamia ratiba maalumu ya wanafunzi katika shule zote za serikali na binafsi ili watoto wapate muda wa kushiriki shughuli zingine, kuimarisha huduma za TEHAMA katika utoaji huduma," alisema.

Naye Msemaji wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Dk. Camilius Kasala, alishauri Dira ihakikishe familia za watanzania zinakuwa na uhakika wa afya kwa kupata bima, chakula na ushirikishwaji wa masuala mbalimbali ya kijamii, zipewe fursa nyezo na ajira ili kuwa na uhakika wa kiuchumi.

Alipendekeza familia kupitia utaratibu wa elimu ya watu wazima iweke utaratibu wa kijihusisha na jamii nyingine, ili iweze kujiamini kushiriki masuala mengine jumuishi yanayolenga kuinua uchumi.

"Pia, ni muhimu vijana wakapewa mazingira, nyenzo na ujuzi utakaowawezesha kufuatilia, kushiriki na kutoa maoni katika kila nyanja, ikiwamo kuwatengenezea ajira zitakazowapatia kipato cha uhakika," alisema.

# TLS yataja dawa kumaliza matukio ya utekaji watu

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kimeshauri serikali iridhie mkataba wa kimataifa wa upotezwaji watu ili kuanzishwe Tume ya Taifa ya Upotezwaji Watu na kupata suluhu ya matukio ya watu kupotea na kutekwa nchini.

Rais wa chama hicho, Wakili Boniface Mwabukusi alitoa rai hiyo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali yanayoendelea nchini kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Alisema kuwapo tume hiyo kutasaidia kutoa kinga na haki kwa waathiriwa wa utekaji na familia zao.

"Suala la utekaji linaendelea kuwa doa jeusi katika historia ya Afrika Mashariki. Kwa sasa hata mtu akipotea kutokana na mambo yake binafsi, taifa linaingia lawamani kwa sababu tayari limetiwa doa," alisema Wakili Mwabukusi.

Alishauri Tanzania irejee katika Mahakama ya Afrika Mashariki ya Haki za Binadamu na Watu ili kutoa nafasi kwa wananchi wake kupata haki kwa wakati ndani ya mipaka na katika ngazi za kimataifa.

Kuhusu Uchaguzi Mkuu ujao, Wakili Mwabukusi alikumbusha kuwa Katiba na sheria ni nyenzo za kulinda demokrasia nchini, hivyo vinapaswa kuzingatiwa.

"Uchaguzi huru na wa haki ni kiashiria cha taifa linalothamini demokrasia na umoja wa wananchi wake.

"Ninatoa wito kwa viongozi wote wa kisiasa kuhakikisha kwamba wanazingatia misingi ya sheria, wanaepuka kuwagawa wananchi na kujenga mazingira ya umoja na utaifa," alisisitiza Wakili Mwabukusi.

Pia alishauri Jeshi la Polisi kulinda wananchi badala ya kuwa sehemu ya Msajili wa Vyama vya Siasa katika kutekeleza majukumu ili kuendelea kuishi katika misingi ya haki na uhuru.

Alikemea tabia za wanasiasa na viongozi wanaotumia lugha za kebehi, udini, jinsia na ukabila kuwabeza wagombea, akisisitiza kuwa tabia hizo zinaligawa taifa na kuwataka wajenge hoja zenye mashiko.

Kuhusu mchakato wa uchaguzi wa ndani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Wakili Mwabukusi alisema kinachoendelea ni ukomavu wa demokrasia uliozidi na kusababisha misuguano.

Alisema kwa ukubwa wa chama hicho, kilipaswa kiwe kinafahamu viongozi wa kuwaongoza katika uchaguzi unaoendelea badala ya watu kuibuka ghafla.

Alisema uchaguzi huo unaakisi kuwa nchini kunahitajika vyama vingi vya kisiasa takribani 600,000 badala ya 19 vilivyopo kulingana na idadi ya watu milioni 60 waliomo nchini.

Pia alitaja sababu za kumuunga mkono mgombea wa CHADEMA anayewania nafasi ya uenyekiti, Tundu Lissu, akisema ni mwanachama mwenzake wa TLS na amekuwa sehemu ya kuhamasisha wanachama wagombee nafasi mbalimbali za uongozi.

Wakili Mwabukusi alisema: "Nimehimiza mawakili wasiridhike na kukaa ofisini, watoke wawanie nafasi za uongozi na hili Lissu amelifanya. Kwanini nisimuunge mkono."

## Raia 16 wauawa na jeshi kimakosa Nigeria

**ABUJA,** Nigeria

RAIA 16 wameuawa katika Jimbo la Zamfara Kaskazini Magharibi mwa Nigeria wakati wa shambulio la anga la jeshi la nchi hiyo, kwa kudhaniwa kuwa ni magenge ya wahalifu.

Wakazi waliambia vyombo vya habari vya ndani jana kuwa waathiriwa walikuwa wanachama wa makundi ya walinzi wa eneo hilo na raia wanaojilinda dhidi ya magenge yenye silaha yanayowateka watu kwa lengo la kupata kikombozi.

Ilielezwa kuwa mashambulizi hayo yalilenga magenge ya wanamgambo katika maeneo ya Zurmi na Maradun na kwamba Gavana wa jimbo hilo, Dauda Lawal, alitoa rambirambi zake kwa jamii.

Jeshi lilikiri kufanya mashambulizi ya angani, ambayo ilisema ni pigo kubwa kwa majambazi wanaovamia vijiji katika eneo hilo.

Jeshi la Anga la Nigeria (NAF) lilisema linachunguza ripoti za kuawa kwa wakazi, japokuwa operesheni hiyo ilifanikiwa kuwaondoa majambazi kadhaa na kusaidia kupatikana kwa baadhi ya waathiriwa wa utekaji.

"NAF inasikitika kuwa raia kadhaa walipoteza maisha wakati wa operesheni," ilisema katika taarifa.

Shirika la habari la AFP lilimnukuu mmoja wa wakazi akisema kuwa raia hao walikuwa wakirejea vijijini mwao baada ya kuwafukuza majambazi waliposhambuliwa kwa mabomu.

Wanakijiji walipata miili 16 kutokana na mashambulizi na kuwapeleka hospitali watu wengine kadhaa waliojeruhiwa vibaya," alisema Sa'idu Ibrahim. **BBC**

## Chama tawala Chad chapata ushindi uchaguzi wa bunge

**N'DJAMENA,** Chad

CHAMA tawala nchini Chad kimepata viti vingi katika uchaguzi wa bunge wa mwezi Desemba, ambao ulisusiwa na vyama vikuu vya upinzani ambako wachambuzi wanasema utaimarisha nguvu za kisiasa za rais.

Ilielezwa kuwa katika uchaguzi wa kwanza wa bunge nchini Chad kipindi cha zaidi ya muongo mmoja, chama tawala Patriotic Salvation Movement kilipata viti 124 kati ya 188, huku idadi ya wapigakura ikiwa asilimia 51.5, kulingana na matokeo ya awali yaliyotangazwa Jumamosi jioni na Ahmed Bartchiret, mwenyekiti wa tume ya uchaguzi.

Uchaguzi wa bunge, pamoja na wa serikali za mitaa na mikoa, ni mwendelezo wa kipindi cha mpito kuelekea utawala wa kidemokrasia baada ya Mahamat Deby kuchukua madaraka kama mwanajeshi mwaka 2021.

Hata hivyo, kiongozi huyo aliingia madarakani baada ya kifo cha baba yake na rais wa muda mrefu Idriss Deby Itno, ambaye aliongoza kwa miongo mitatu. Deby alishinda uchaguzi wa rais wenye utata wa mwaka jana. **VOA**

# Mtanzania aliyetekwa nyara Kenya aachiliwa

**NAIROBI, Kenya**

MWANAHARAKATI wa haki za binadamu Tanzania, Maria Sarungi ameachiliwa baada ya kutekwa nyara kwa saa kadhaa akiwa Kenya, ambako video iliyochapishwa kwenye ukurasa wake wa X, amethibitisha kuwa alitekwa huku akaahidi kutoa maelezo zaidi baadaye.

Shirika lake la Amnesty International lilisema Sarungi alitekwa nyara katika mitaa ya mji mkuu wa Kenya Nairobi, ambako katika video iliyochapishwa jana Sarungi alionekana akiwa ameambatana na watu wengine wanne, aliangua kilio akisema sasa yuko salama.

"Asanteni sana, niko salama, Mungu ni mwema na kesho nitachukua muda niwashukuru vizuri, nawashukuru watu wa Kenya, watu wa Tanzania na Kimataifa. Natoa shukrani zaidi kwa walionipigania, kwasababu leo nimeweza kuokolewa salama," alisema Sarungi.

**Shirika lake la Amnesty International lilisema Sarungi alitekwa nyara katika mitaa ya mji mkuu wa Kenya Nairobi, ambako katika video iliyochapishwa jana Sarungi alionekana akiwa ameambatana na watu wengine wanne, aliangua kilio akisema sasa yuko salama.**

Ilielezwa kuwa Sarungi anafanya kampeni za mabadiliko ya kisiasa, uhuru wa kujieleza na haki za wanawake nchini Tanzania.

Shirika la Amnesty tawi la Kenya lilisema alitekwa nyara na watu watatu waliokuwa na silaha kwenye gari nyeusi (Toyota) Noah majira ya saa tisa mchana katika eneo la Kilimani katikati mwa Nairobi. **TRT**



Mkutano wa mawaziri wa kigeni wa Ulaya na Uarabuni kuhusu Syria ukifanyika mjini Riyadh, Saudi Arabia jana. **PICHA: MTANDAO.**

# Rais Zelensky aonyesha yuko tayari kubadilishana wafungwa na Russia

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky amesema yuko tayari kuwarejesha nchini mwao wanajeshi wawili wa Korea Kaskazini waliotekwa, kwa mabadilishano ya kuachiliwa huru wafungwa wa kivita raia wa Ukraine walioko Russia.

Pendekezo la Zelensky alilitoa saa chache baada ya idara ya kitaifa ya ujasusi ya Korea Kusini kuthibitisha tangazo la siku iliyopita kwamba Ukraine imewakamata wanajeshi wawili wa Korea Kaskazini.

Mamlaka nchini Ukraine Jumamosi ilisema wanajeshi hao wawili walijeruhiwa vibaya katika uwanja wa vita wakati wakipambana na wanajeshi wa Ukraine katika eneo la Kursk nchini Russia, lakini wakati huo hawakutoa ushahidi kuthibitisha uraia wao.

Hata hivyo, Jumapili, Idara ya Ujasusi ya Korea Kusini (NIS) imeliambia AFP kwamba, imethibitisha kuwa jeshi la Ukraine limewakamata wanajeshi wawili wa Korea Kaskazini Januari 9, mwaka huu, katika uwanja wa vita eneo la Kursk, nchini Russia.

Zelensky aliandika katika mtandao wa kijamii wa X kwamba wanajeshi wa Korea Kaskazini ambao hawataki kurudi nyumbani na wanaoonyesha nia ya kuleta amani kwa kueleza ukweli kuhusu vita hivyo nchini mwao, watapewa kile alichokiita fursa nyingine.

Alipoulizwa mwaka jana kuhusu ushiriki wa wanajeshi wa Korea Kaskazini, Rais wa Russia Vladimir Putin hakukiri wala kukanusha kwamba nchi hiyo inatumia wanajeshi wa Korea Kaskazini katika vita vyake dhidi ya Ukraine.

Aidha, Ukraine, Marekani na Korea Kusini zimeishtumu Korea Kaskazini, nchi yenye silaha za nyuklia kwa kutuma wanajeshi zaidi ya 10,000 kulisaidia jeshi la Russia katika vita vyake dhidi ya Ukraine.

Ilielezwa kuwa nchi hizo na Korea Kaskazini, zimeimarisha ushirikiano wao wa kijeshi tangu Moscow ilipoivamia Ukraine mwaka 2022.

Hata hivyo, ikulu ya Marekani White House imesema idadi kubwa ya wanajeshi wa Korea Kaskazini wameuawa vitani.

Inaelezwa kuwa Desemba 2024 shirika la ujasusi la Korea Kusini liliripoti juu ya kukamatwa kwa mwanajeshi wa kwanza wa Korea Kaskazini na vikosi vya Ukraine japo baadaye alifariki dunia.

"Hakuna shaka yoyote duniani kwamba Jeshi la Russia linategemea msaada wa kijeshi kutoka Korea Kaskazini," alisema Zelensky.

Rais huyo wa Ukraine alichapisha video inayoonyesha wanajeshi wawili wa Korea Kaskazini waliotekwa wakihojiwa. Mmoja akionekana amelala kwenye kitanda huku mwengine akiwa ameketi kitandani na bandeji shingoni.

**DW**

# ZIDANE AWATAKA MASHABIKI AZAM KUKAA MKAO WA KULA

Na Adam Fungamwango

KIUNGO mshambuliaji mpya wa Azam FC, Zidane Sereri, amewataka mashabiki wa klabu hiyo, kusubiria mambo mazuri kutoka kwake, pale utakapoanza mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Machi, mwaka huu.

Sereri alisema hayo jana, siku moja tu baada ya kutangazwa kusajiliwa na Azam FC kwa mkataba wa miaka mitano, utakaomalizika 2030.

"Nina furaha kubwa kujiunga na klabu kubwa kama Azam FC, ni moja ya klabu kubwa nchini, naamini nitakuwa kwenye wakati nzuri, nawaambia mashabiki wa timu hii wakae mkao wa kula kwani mambo mengi mazuri yanakuja," alisema mchezaji huyo ikiwa ni kauli yake ya kwanza kwa vyombo vya habari tangu atangazwe kujiunga na klabu hiyo.

Sereri amejiunga na Azam, akitoka Dodoma Jiji, ambako amecheza kwa kiwango kikubwa kwenye mzunguko wa kwanza, akiwa na mabao mawili mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Unakuwa ni usajili wa pili kufanyika kwa klabu hiyo, kwani siku chache zilizopita ili msajili beki wa kati raia wa Ivory Coast, Zouzou Landry kutoka Klabu ya AFAD Djekanou ya nchini humo.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu hiyo, Thabit Zacharia, amesema usajili unaofanyika ni kwa matakwa ya Kocha Mkuu, Rachid Taoussi, ambaye alihitaji marekebisho madogo kwenye kikosi chake.

Azam, tayari imeshaanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, huku kila wiki ikitarajia kucheza michezo ya kirafiki ya ndani.

"Tulianza mazoezi tangu Jumatatu ya wiki iliyopita, kujiandaa na mechi za mzunguko wa pili, tunaendelea hivi na mazoezi, lakini kila baada ya wiki moja tutakuwa tunacheza michezo ya kirafiki.

Nia ni kuangalia jinsi gani tunapiga hatua. Huwezi kufanya tu mazoezi kila siku halafu hujui umefikia wapi, ndiyo maana kocha wetu akasema kuwa anahitaji kufanya mazoezi kila siku baada ya mazoezi hadi pale Ligi Kuu itaporejea tena mwezi Machi," alisema Zakazi.

Hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, Azam ipo kwenye nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi Kuu ikikusanya pointi 36, ikicheza michezo 16, kushinda 11, sare tatu, ikipoteza mechi mbili.

# Tenesi Taifa Vijana yataka taji Kenya

Na Shufaa Lyimo

KIKOSI cha wachezaji 12 wa Timu ya Taifa ya Vijana ya Tanzania ya Mchezo wa Tenesi, kimeondoka jana, Jumatatu kuelekea Nairobi, Kenya kushiriki mashindano ya Afrika yatakayoanza kutimua vumbi kesho nchini humo huku kikiwa na matumaini makubwa ya kurejea na taji.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salum Mvita, alisema mashindano hayo yatashirikisha timu za wanaume pamoja na wanawake.

Alisema maandalizi kuelekea katika mashindano hayo yanaendelea vema na kwamba malengo yao ni kwenda kuipeperusha vizuri bendera ya Tanzania.

"Malengo yetu ni kupata ushindi kwenye mashindano hayo ili tuweze kuipeperusha vema bendera ya Tanzania, alisema Mvita.

Mvita alisema wamefanya mazoezi kwa muda mrefu ambayo anaamini yatawasaidia wachezaji wake hao kufanya vizuri.

MUZIKI...



Mwalimu wa muziki kutoka Kanisa la Waadventista Wasabato Mbezi Luis, Dar es Salaam, Jovin Tongora (kushoto), akiendesha somo la muziki na falsafa za muziki wa kanisa kwa waumini wa kanisani hapo juzi. Somo hilo ni sehemu ya programu maalum iliyoandaliwa na kanisa hilo ili kuimarisha na kuinua huduma yake ya muziki. **MPIGAPICHA WETU**

# TMA yatimua kocha Mtibwa, Geita ni moto

Na Adam Fungamwango

KLABU ya TMA Stars, imetangaza kuachana na kocha wake, Maka Mwalwisi siku moja tu baada ya kupokea kichapo cha mabao 3-2 kutoka kwa Bigman FC, mechi iliyochezwa, Uwanja wa Ilulu, Lindi.

Taarifa iliyotolewa jana kutoka Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, imeeleza kuwa imeamua kusitisha mkataba kwa makubaliano ya pande mbili.

"Uongozi wa timu ya TMA Stars, unapenda kuwatangazia kuwa, umefikia makubaliano ya pande mbili kusitisha mkataba wa kazi na kocha Mwalwisi.

"Klabu inapenda kutoa shukrani kwa kocha huyo kutokana na mchango wake na tunamtakia kila la heri na tayari mchakato wa kutafuta kocha umeshaanza na unatarajiwa kukamilika hivi punde," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Kocha huyo amewahi kuzifundisha klabu mbalimbali za Ligi Kuu, zikiwamo Mbeya City na Mbeya Kwanza.

TMA, yenye maskani yake jijini Arusha ipo nafasi ya tano ya msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na pointi 27 kwa michezo 15 iliyocheza mpaka sasa.

Wakati hayo yakiendelea, timu zilizoshuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu uliopita, Mtibwa Sugar na Geita Gold, zimeendeleza vichapo kwenye ligi hiyo iliyoendelea juzi.

Kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Geita, timu ya Geita Gold, iliiadhibu Stand United mabao 3-1, huku Mtibwa Sugar ikiwa ugenini, Uwanja wa Mbatini, Mlandizi mkoani Pwani, ilipata ushindi wa bao 1-0 na kuendelea kujikita kileleni.

Bao pekee kwenye mchezo huo lilifungwa na Erick Kyaruzi, dakika ya 52 na kuifanya kufikisha pointi 38 baada ya kucheza michezo 15.

# Muya abebeshwa zigo zito Geita Gold

Na Mwandishi Wetu

KOCHA wa zamani wa Fountain Gate, Mohamed Muya, amejiunga na Klabu ya Geita Gold, akipewa malengo ya kuhakikisha anaipandisha Ligi Kuu Tanzania Bara msimu unaokuja.

Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Leonard Bugomola, amebainisha kuwa moja ya malengo waliyompa ni kuhakikisha timu inarejea tena Ligi Kuu.

"Tunaamini kwa uwezo alionao kocha huyo ataifikisha timu kwenye malengo tuliyokusudia ya kurejea tena Ligi Kuu, hilo hatuna wasiwasi nalo," alisema mwenyekiti huyo.

Geita Gold inapigana kutaka kurejea tena Ligi Kuu baada ya kuteremka msimu uliopita ambapo kwa sasa iko nafasi ya tatu ya msimamo ikiwa na pointi 33 kwenye ligi ya Championship, nyuma ya Mbeya City yenye alama 34 na Mtibwa Sugar inayoongoza kwa pointi 38.

Muya, amechukuliwa na timu hiyo baada ya kutimuliwa na Fountain Gate, dakika chache tu baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga, Desemba 29, mwaka jana, timu yake ikipata kipigo cha mabao 5-0, mechi ikichezwa, KMC Complex, Dar es Salaam.

Fountain Gate, tayari imemtangaza raia wa Kenya, Robert Matano kama Kocha Mkuu, akisaidiwa na Amri Said.

Klabu hiyo imeamua kumchukua Muya baada ya kuachana na Kocha wao, Amani Josiah aliyekwenda kujiunga na Maafande wa Prisons, ambayo nayo ilitoka kuachana na Kocha wake, Mbwana Makata.

## ZISIKUPITE

### GARNACHO ATAKIWA NAPOLI

KOCHA wa Napoli, Antonio Conte, anamtaka winga wa Manchester United, Alejandro Garnacho mwenye umri wa miaka 20, kuchukua nafasi ya winga wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia (23), ambaye anatarajiwa kuhamia Paris St-Germain. ***(Sport Italia)***

### ARAUJO ATAKA KUONDOKA

MLINZI wa Uruguay, Ronald Araujo, ambaye amekuwa akihusishwa na Juventus, anataka kuondoka Barcelona haraka iwezekanavyo, lakini klabu hiyo ya Katalunya ina nia ya kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. (***Mundo Deportivo***)

### HUMMELS HANA HARAKA

BEKI wa Ujerumani, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 36, hana haraka ya kuanza mazungumzo juu ya kuongezwa kwa mkataba wake katika Klabu ya AS Roma, huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kukamilika mwezi Juni. ***(Soka Italia)***

### WEST HAM KULETA STRAIKA

KLABU ya West Ham iko tayari kuleta mshambuliaji mpya baada ya kujua ukubwa wa jeraha la msuli wa mshambuliaji wa Ujerumani, Niclas Fullkrug mwenye umri wa miaka 31, alilopata katika mechi ya Ijumaa ya Kombe la FA dhidi ya Aston Villa. (***Fabrizio Romano)***

### ALVAREZ HAONDOKI WEST HAM

MONACO imewasilisha ombi la kumnunua kiungo wa West Ham, Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 27, baada ya ofa ya kumsajili kwa mkopo mchezaji huyo wa Kimataifa wa Mexico kukataliwa na West Ham. (***Fabrizio Romano***)

### FERGUSON NAYE AHUSISHWA

MSHAMBULIAJI wa Brighton ya Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 20, na mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford (27), wamehusishwa na uhamisho wa mkopo kwenda West Ham. (***TBR Football***)

### CALVERT-LEWIN NA ATALANTA

KLABU ya Atalanta inataka kukamilisha usajili wa Januari wa mshambuliaji wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27, ambaye amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kuelekea Newcastle United msimu wa majira ya joto kwa uhamisho wa bure. (***Sun***)

### DAVIES MKATABA MPYA

KLABU ya Bayern Munich imempa mlinzi wa Canada, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 24, mkataba mpya wenye thamani ya euro milioni 25, huku Real Madrid ikipania kumsajili kwa uhamisho wa bila malipo msimu wa majira ya joto. ***(Marca)***

### NUAMAH ATAKIWA EVERTON

KLABU ya Everton inafikiria kuwasilisha ombi la kumnunua winga wa Lyon raia wa Ghana, Ernest Nuamah, 21. (***RMC Sport)***

### COULIBALY KWA LEICESTER

LEICESTER City imekubali dili la kumsajili beki wa pembeni wa Ufaransa, Woyo Coulibaly mwenye umri wa miaka 25, kutoka Parma. (***Gianluca di Marzio***)

### CARLOS ATAJWA FENERBAHCE

KLABU ya Fenerbahce imefanya mazungumzo na Aston Villa kuhusu mkataba wa pauni milioni 10 kwa beki wao wa kati Mbrazil, Diego Carlos, 31. (***Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AKUBALI KWA UTD HESABU SASA KWA SPURS

**LONDON,** England

**Katika michezo elfu moja, unapaswa kupoteza mmoja na labda ulikuwa huu, hivyo...**

MIKEL Arteta alielezea kutolewa kwa Arsenal katika raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Manchester United Jumapili kama ni pigo baada ya kushindwa kwa mikwaju ya penalti kwenye Uwanja wa Emirates.

**Bruno Fernandes aliwawe ka wageni mbele dakika ya 52 kabla ya Diogo Dalot ku tolewa kwa kadi nyekundu dakika tisa baadaye kwa kumchezea rafu Mikel Me rino.**

Gabriel Magalhães alisawazisha dakika ya 63, lakini licha ya kucheza karibu saa moja dhidi ya wachezaji 10, Arsenal hawakuweza kupata bao lingine, huku nahodha Martin Ødegaard akikosa penalti dakika 18 za mwisho.

United waliona haki haikutendeka kutokana na mkwaju huo wa penalti kutolewa licha ya Harry Maguire kuonekana kutomchezea rafu Kai Havertz kwenye eneo la hatari (hakuna VAR kwenye Kombe la FA hadi raundi ya tano).

Lakini United walijikuta wakitumia muda mwingi kulinda lango lao kwa muda mrefu baadaye, wakati Arsenal wakitafuta ushindi.

Wenyeji walisajili mikwaju 26 kwa jumla, huku Havertz akikosa nafasi nyingi za wazi.

Pia alikuwa mchezaji pekee aliyekosa penalti, Altay Bayindir aliokoa mkwaju wake na kumpa Joshua Zirkzee nafasi ya kufunga na sasa watacheza na Leicester City raundi ya nne.

"Haiwezekani," alisema Arteta akiiambia BBC Sport.

"Ni wazi, unapima kiwango cha ufaulu na tulichokifanya kuhusiana na nafasi hiyo, unajua, unastahili kushinda. Lakini ukweli ni kwamba tumetoka.

"Nawapenda wachezaji wangu. Ninaipenda timu yetu na napenda jinsi walivyo wazuri na wanachofanya kwa sababu katika michezo elfu moja, unapaswa kupoteza mmoja, na labda ulikuwa huu.

"Unapaswa kuelewa hili pia, ni sehemu ya sekta yetu, mchezo wetu na songa mbele kwa sababu huna muda wa kufanya hivyo, kwa sababu Jumatano tuna mchezo mkubwa."

Arsenal wanakabiliwa na mechi ya Ligi Kuu England nyumbani dhidi ya Tottenham, kesho, Jumatano.

# FLICK AJIVUNIA KIKOSI BARCA KUIUA MADRID



**JEDDAH,** Saudi Arabia

HANSI Flick amesema "najivunia sana" kwa uchezaji "wa ajabu" kutoka kwa timu yake ya Barcelona, baada ya kutoka nyuma na kuifunga Real Madrid mabao 5-2 katika fainali ya Supercopa ya Hispania iliyopigwa Saudi Arabia Jumapili.

Kylian Mbappe alianza kuiweka mbele Madrid kwa bao lake la dakika ya tano kwenye Uwanja wa Al Jawhara mjini Jeddah, lakini mchezo ukaugeuka kwa mabao ya Raphinha, Lamine Yamal, Robert Lewandowski na Alejandro Balde.

"Ninajivunia sana," alisema Flick katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Ninajivunia timu, benchi la ufundi, klabu, mashabiki na kila mtu. Leo (juzi) ilikuwa mechi ya kushangaza. Kwa makocha, si sana! Lakini kwa mashabiki ni nzuri sana."

Kikosi cha Flick kilianza msimu kwa nguvu na kilikuwa kinaongoza LaLiga kabla ya mwenendo mbaya Novemba na Desemba na kiliwafanya wapoteze pointi katika mechi sita kati ya saba za mwisho za ligi, huku mbinu za Flick zikitiliwa shaka.

"Lazima tujifunze kutoka katika kila mechi," alisema Flick alipoulizwa nini maana ya ushindi wa Supercopa kwa kipindi kizima cha msimu.

"Tunaweza kufanya mambo vizuri zaidi, lakini tuna timu changa. Tulikuwa na wiki kadhaa ambapo hatukufanya vizuri, na hali yetu kwenye ligi sasa si nzuri. Tunazungumza mambo haya yote kwenye chumba cha kubadilishia nguo, lakini kwangu ni muhimu kuzingatia mechi ijayo."

"Tunajua tunachopaswa kufanya uwanjani," alisema nahodha Raphinha katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi, huku akitajwa kuwa mchezaji bora wa fainali hiyo.

"Jambo muhimu ni sisi kuweza kupigania mataji na kuyashinda."

Licha ya kucheza na wachezaji 10 kwa dakika nyingi baada ya kipa Wojciech Szczesny kuoneshwa kadi nyekundu, uongozi wa Barcelona haukuonekana kuwa hatarini.

Szczesny alianza michezo yote miwili kwenye Supercopa, baada ya kipa Iñaki Peña kuachwa baada ya kuchelewa kuwasili kwenye mkutano wa timu.

"Wakati Wojciech alipotolewa nje kwa kadi nyekundu, haikuwa rahisi kwetu," alisema Flick.

"Iñaki alifanya vema, kutoka sifuri hadi shujaa. Lakini ninajivunia jinsi tulivyolinda, kila hali, kulinda goli kama timu moja."

Huu ni ushindi wa pili kwa Barcelona wa Clasico msimu huu baada ya kushinda mabao 4-0 Oktoba, mwaka huu.

"Sitaki kuangalia nyuma," Flick alisema.

"Leo (juzi) ni siku nzuri, tumeifunga moja ya timu bora zaidi duniani, kwa mara ya pili msimu huu."

# AC Milan yaongoza kumtwaa Walker

**MILAN,** Italia

AC Milan inaongoza mbio za kumsaka Kyle Walker, vyanzo vimeiambia ESPN, baada ya kuiambia Manchester City kuwa anataka kuondoka katika klabu hiyo.

Walker aliachwa nje ya kikosi kilichoshinda mabao 8-0 Kombe la FA dhidi ya Salford City Jumamosi baada ya kumfahamisha Mkurugenzi wa Soka, Txiki Begiristain, kwamba anataka kuhamia nje ya nchi katika dirisha la Januari hii.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alikuwa karibu kujiunga na Bayern Munich mwaka wa 2023.

Ana mkataba hapo kwenye Uwanja wa Etihad hadi 2026, lakini chanzo kimeiambia ESPN kwamba Milan wako tayari kumpa Walker mkataba hadi 2027.

"Nilimwambia sasa ni suala la soko," alisema Guardiola.

"Ni mchezaji wa ajabu mwenye umbile lake la ajabu, anapokuwa makini hawezi kuzuilika kama beki wa kulia, ni mchezaji wa daraja la juu, kama yuko fiti anaweza kucheza mwaka mmoja, miwili, mitatu au minne zaidi.

"Sijawahi kuona mchezaji mwenye hali hizi za kimwili katika maisha yangu ya soka, na bila shaka, lakini lazima awe na makubaliano na klabu."


Guardiola alifichua kutokuwa na uhakika juu ya mustakabali wa Walker ulimaanisha kuachwa nje ya kikosi kilichomenyana na Salford City na dhidi ya Brentford kwenye Ligi Kuu England Jumanne na Guardiola alisema Walker anaweza kukosa tena.

"Sijui, inategemea jinsi tutakavyofanya mazoezi," alisema Guardiola.

"Nadhani nilikuwa wazi wakati wote, ikiwa anataka kuchunguza, klabu itachunguza, na anapaswa kuamua, si mimi. Si uamuzi wangu."



# Jorginho kuondoka Arsenal Januari hii




**LONDON,** England

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Jorginho, anaweza kuondoka katika klabu hiyo wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari hii ni kutokana na kukosa muda wa kutosha wa kucheza, kwa mujibu wa ripoti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ameingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na Arsenal baada ya kujiunga na klabu hiyo katikati ya msimu wa 2022/23 kutoka kwa wapinzani wao wa London Chelsea kwa pauni milioni 12, na inaonekana kuna uwezekano mkubwa wa kupewa mkataba mpya.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Italia mwenye michezo 57, amekuwa akitumiwa kwa kiasi kidogo na Mikel Arteta msimu huu na ameanza mara tisa tu katika mashindano yote, na kumuacha akichanganyikiwa kwa kukosa nafasi katika kikosi cha kwanza.

Kwa mujibu wa ESPN, Jorginho sasa anafikiria kuondoka na amepewa ofa kwa Klabu ya Brazil, Palmeiras baada ya mkutano kati ya wakala wa mchezaji huyo na Arsenal.

Palmeiras na Flamengo ndizo klabu mbili ambazo Jorginho, ambaye alizaliwa nchini Brazil licha ya kuiwakilisha Timu ya Taifa ya Italia, anafikiria kujiunga nayo wakati wa dirisha la majira ya baridi.

Arsenal huenda ikashawishiwa kumuuza kiungo huyo Januari hii kabla ya kuondoka bila malipo msimu wa majira ya joto.

'Washikabunduki' hao bado wanawania taji la Ligi Kuu England licha ya kukaa pointi sita nyuma ya vinara wa ligi, Liverpool, lakini wamekuwa kwenye wakati mgumu katika ubunifu na msukumo wa mashambulizi katika wiki za hivi karibuni - suala lililozidishwa na jeraha la muda mrefu la Bukayo Saka.

HABARI MICHEZO

## Ramovic arudi na dawa ya MC Alger

INATOKA UKURASA 24

juzi ulikuwa mgumu na wenye presha kubwa kwao, lakini kwa bahati nzuri wakaibuka kuwa washindi.

"Haikuwa mechi rahisi, lakini tumeweza, nawapongeza wachezaji wangu na viongozi, ulikuwa mchezo mzuri uliokuwa na presha kubwa kwetu, umetuonesha kuwa sisi ni watu wa aina gani, tumeonesha kuwa sisi ni wapambaji.

"Tungeweza kupata bao la pili kipindi cha pili, lakini tukakosa kutumia nafasi. Sasa tunarudi Tanzania kwenye uwanja wetu kwa mchezo dhidi ya MC Alger, hautokuwa mwepesi, lakini tutapambana," alisema kocha huyo.

Ushindi huo umeifanya Yanga kufikisha pointi saba, ikiendelea kuwa nafasi ya tatu nyuma ya MC Alger ambayo ni ya pili ikiwa na pointi nane, huku kundi hilo likiongozwa na Al Hilal yenye pointi 10, na tayari imeshafuzu hatua ya robo fainali.

Mabingwa hao wa Tanzania Bara, watacheza mchezo wao wa mwisho wa hatua ya makundi Jumamosi ijayo dhidi ya MC Alger kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, saa 10:00 alasiri, ikitakiwa kushinda tu kwa idadi yoyote ya mabao ili iweze kusonga mbele.

Ikishinda itafikisha pointi 10 na kuwaacha Waalgeria hao wakisalia na pointi nane, lakini sare yoyote itaifanya kufikisha pointi nane hivyo kushindwa kufuzu kwani MC Alger itakuwa imefikisha alama tisa.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amesema hautokuwa mchezo rahisi kwa sababu wapinzani wao watakuja kwa nguvu ili kupata matokeo mazuri, kwani matokeo ya ushindi na sare yoyote yatawawezesha kufuzu.

"Kwetu sisi hatuna njia nyingine ya kufuzu robo fainali zaidi ya kuwagaragaza pale Benjamin Mkapa, tuko tayari kupambania hiyo heshima," alisema Kamwe.

# TABORA UTD YANASA MKATA UMEME KUTOKA CAMEROON

**Na Adam Fungamwangu**

SIKU chache kabla ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili, Klabu ya Tabora United, imefanikiwa kumsajili kiungo mkabaji raia wa Cameroon, Cedric Martial Zamba, kutoka timu ya Touarga ya Morocco.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imeeleza kuwa usajili huo ni wa kwanza kutangazwa rasmi na klabu hiyo, na umefanyika kwa mapendekezo ya Kocha Mkuu, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Anicet Kiazayidi.



Mshambuliaji wa Yanga, Prince Dube, akijaribu kufunga kwenye mchezo wa Kundi A Ligi ya Mabigwa Afrika dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan uliochezwa Uwanja wa De la Capitale, jijini Nouakchott nchini Mauritania juzi usiku. Yanga ilishinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

"Tumempata mchezaji mpya ambaye ni kiungo mkabaji raia wa Cameroon, anayekuja kusaidiana na wachezaji waliopo katika kuendeleza gurudumu la timu yetu na malengo yetu," ilieleza sehemu ya taarifa ya klabu hiyo jana.

Mbali na kiungo huyo, taarifa zinaeleza kuwa klabu hiyo ipo kwenye mazungumzo ya mwisho na kipa raia wa Gabon, Jean Noel Amonone, ambaye amezidakia Klabu za Amazulu ya Afrika Kusini na AS Arta Solar ya Djibouti, huku mara kwa mara akiwa anaitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya nchi hiyo.

Wakati kipa huyo akitajwa kutua Tabora United, pia anatajwa kipa Fikirini Bakari kwenda kusaidiana naye, baada ya Klabu ya Singida Black Stars kuamua kumrejesha kipa wake, Hussein Masalanga.

Fikirini, kipa wa Singida, alichezea Fountain Gate mechi za mzunguko wa kwanza kwa mkopo, huku Masalanga naye akiichezea Tabora United kwa mkopo.

Ofisa Habari wa Singida Black Stars, Hussein Massanza, amekiri kujereshwa kundini kwa Masalanga baada ya kuichezea Tabora United kwa mkopo wa miezi sita akieleza sababu ni kiwango bora alichokionesha mechi za mzunguko wa kwanza.

Kutokana na hali hiyo, Singida, wameamua kumpeleka Tabora United, Fikirini, kipa aliyerudishwa na Fountain Gate kwa kile kilichodaiwa kutoridhishwa na uwezo katika mchezo dhidi ya Pamba Jiji uliofanyika Novemba 5, mwaka jana katika Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Manyara, akiigharimu timu yake kufungwa mabao 3-1.

# Fadlu sasa ataka ukinara wa kundi

INATOKA UKURASA 24

wangu kwenye benchi la ufundi pamoja na madaktari wangu, wote hawa wamefanya kazi kubwa sana.

"Kwa sasa tunaangalia mechi ya mwisho, tunataka kushinda ili kuongoza kundi, umuhimu wa mchezo wa mwisho ni mkubwa sana, kwani tutapata faida ya kuanzia ugenini, ukifanikiwa kuwabana wapinzani wako kwao, halafu ukamalizia nyumbani, unakuwa na faida kubwa, kama tunataka kuvunja rekodi yetu ya kufuzu hatua ya nusu fainali, ushindi dhidi ya CS Constantine ni muhimu sana," alisema Fadlu.

Simba itacheza mchezo wa mwisho Jumapili ijayo dhidi ya CS Constantine katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, saa 10:00 alasiri, mechi ambayo inahitaji ushindi ili ifikishe pointi 13, na kuwaacha wapinzani wao na pointi zao 12 kama inataka kuwa kinara wa Kundi A.

Akizungumzia mchezo huo, alisema walimiliki mpira kwa kiasi kikubwa huku wapinzani wao wakitegemea zaidi mashambulizi ya kushtukiza na mipira iliyokufa tu.

"Tumefanya makosa, tumewapa bao, lakini muda mwingi wa mchezo tumekuwa bora, tumepiga mashuti 26 langoni mwao, tumemiliki kwa asilimia 56.

"Wapinzani wetu walikuwa hatari zaidi kwenye mipira ya faulo na kushambulia kwa kushtukiza tu, hawakuwa na kitu kingine zaidi ya nafasi ya bao tulilowapa," alisema.

Hii ni mara ya sita kwa Simba kufuzu hatua hiyo kwa misimu saba ya michuano ya CAF tangu 2018.

Rekodi zinaonesha kuwa tangu msimu wa 2018/19, Simba imekosa kutinga hatua hiyo msimu wa 2019/20 tu ilipotolewa hatua ya awali na UD Songo ya Msumbiji, lakini baada ya hapo imekuwa ikitinga hatua za robo fainali, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, mara tano mfululizo.

Imetinga Ligi ya Mabingwa Afrika mara nne, 2018/19, 2020/21, 2022/23 na 2023/24, huku msimu wa 2021/22 na 2024/25 ikitinda robo fainali Kombe la Shirikisho Afrika.

"Tumefanikiwa kudumisha utamaduni wetu wa kutinga hatua ya robo fainali si jambo dogo, wachezaji wanaingia na kutoka, wengine wanapungua viwango, lakini taasisi imeweza kusimamia mwendelezo huu jambo ambalo si dogo, ukiangalia tangu kipindi chote hicho mpaka sasa timu ambazo zimeweza kuwa na mwendelezo wa kiwango hiki hazizidi tatu, labda Al Ahly, na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, zingine zinaingia na kutoka, angalia Wydad Casablanca na baadhi ya nyingine kuwa hazipo kwenye hatua hii msimu huu," alisema Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally.

Wakati huo huo, beki Fondoh Che Malone, ameomba radhi wanachama na mashabiki wa Simba kutokana na kosa alilofanya lililosababisha bao la kwanza kwa Bravos do Maquis, kabla ya Leonel Ateba kusawazisha.

"Ningependa kuomba msamaha kwa familia nzima ya Simba kwa kusababisha madhara mara mbili kwenye mechi za kimataifa.

"Nabeba lawama kwa makosa yangu, na naahidi kufanya kazi kwa bidii ili kufanya vizuri zaidi katika siku zijazo. Ninaomba radhi kwa dhati. Asante Simba. Asanteni mashabiki kwa kunitia moyo kila wakati licha ya makosa yangu," alisema beki huyo wa kati raia wa Cameroon.

Michezo
Jumanne Januari 14, 2025
Nipashe




Flick ajivunia kikosi Barca kuiua Madrid UKURASA 22




Picha mbili tofauti zikionesha Kiungo mshambuliaji wa Simba, Elie Mpanzu, akiachia shuti kali huku akiwa amezingirwa na 'kijiji' cha wachezaji wa Bravo do Maquis, katika mchezo wa Kundi A Kombe la Shirikisho Afrika uliopigwa Uwanja Novembro 11, Luanda nchini Angola juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. Picha ya pili kulia ni Kibwana Shomari naye akiachia shuti mbele ya mchezaji wa Al Hilal Omdurman ya Sudan kwenye mechi ya Kundi A Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa Uwanja wa De la Capitale, jijini Nouakchott, Mauritania juzi usiku na Yanga kushinda bao 1-0.

# *Fadlu sasa ataka ukinara wa kundi*

## ●●● Simba ikitinga robo fainali ya sita ndani ya miaka saba, Che Malone aomba radhi kwa...

**Na Adam Fungamwango**

SARE ya bao 1-1 iliyoipata Simba kwenye Uwanja wa Novembro 11, Luanda nchini Angola juzi dhidi ya Bravos do Maquis, imeifanya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa mara sita ndani ya misimu saba, huku Kocha Kuu, Fadlu Davids, akisema kazi haijaisha kwani lengo la pili ni kushinda mchezo wa mwisho dhidi ya CS Constantine ya Algeria na kuongoza kundi.

Akizungumza baada ya kutamatika kwa mchezo huo wa Kundi A Kombe la Shirikisho Afrika, Fadlu raia wa Afrika Kusini, alisema kufuzu lilikuwa lengo la kwanza, la pili ni kushinda mchezo ujao kwa sababu moja tu, ya kuongoza kundi kitu ambacho kitakuwa faida kubwa kwa timu hiyo.

Alisema mara kwa mara Simba huishia hatua ya robo fainali kwenye mechi za kimataifa zinazoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), hivyo kama safari hii ikiongoza kundi itakuwa na nafasi nzuri na kuanzia ugenini na kumalizia nyumbani, kitu ambacho kinaweza kuwa faida kubwa ya kuweza kutinga hatua ya nusu fainali.

"Nawapongeza Wanasimba wote kwa kuweza kufuzu kutinga hatua ya robo fainali. Tulitaka kufuzu kabla ya mchezo mmoja na tumeweza kufanya hivyo, nawashukuru sana wasaidizi

INAENDELEA UK. 23

# Ramovic arudi na dawa ya MC Alger

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan uliochezwa Uwanja wa De la Capitale, jijini Nouakchott, nchini Mauritania juzi usiku, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema kazi iliyobaki ni moja tu kushinda mchezo wa mwisho dhidi ya MC Alger ya Algeria, akisema kazi ya kuisoma kuifanyia ushushushu timu hiyo, imeanza mara moja.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo, ambao Yanga ilipata bao pekee kupitia kwa kiungo mshambuliaji wake raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, Ramovic, alisema kwa sababu mchezo huo ni lazima washinde ili kufuzu robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutoka Kundi A, mara moja wameanza kuifuatia MC Alger staili yao ya uchezaji, vitu mbalimbali vya kiufundi, tabia zao, na hasa wanapocheza wakiwa ugenini.

"Tunaendelea kuwasoma MC Alger ili tujue jinsi gani ya kukabiliana nao, tumekuwa tukiangalia mambo mbalimbali ya kiufundi, mfumo wao, staili ya uchezaji, na tutakapofika nyumbani tutaanza kufanya mazoezi ya kile ambacho tumekifanyia kazi," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

Alisema mchezo wa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002